Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# TAKWIMU ZA HALI YA UHALIFU NA MATUKIO YA USALAMA BARABARANI JANUARI – JUNI 2025

OKTOBA 2025

***DIRA***
*Kuwa jeshi lenye weledi katika kudumisha usalama wa watu na mali zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

***DHIMA***
*Kutoa huduma bora zitakazowezesha kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

***DHAMIRA***

***Weledi***
*Kufanya kazi kwa kujitoa, Nidhamu na kuwa na matarajio.*

***Uzalendo***
*Kuwa jasiri, Mwaminifu na Mtiifu kwa nchi*

***Uadilifu***
*Kuwa Mwaminifu, Kutokuwa na upendeleo na ubadhirifu*

***Ubunifu***
*Kuwa mdadisi, Mbunifu, kufanyakazi kwa ufanisi na kujifunza*

***Heshima***
*Kufanya kazi kwa kuheshimiana, kuwa na Umoja upendo na Amani*

***Kaulimbiu***
*Nidhamu, Haki, Weledi na Uadilifu, Msingi wa mafanikio yetu.*

Imetayarishwa na

Inspekta Jenerali wa Polisi,
Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Tanzania,
4 Mtaa wa Posta,
S.L.P. 961,
40483 DODOMA.

Simu: +255 (026) 232385
Nukushi: +255 (026) 232386
Tovuti: www.polisi.go.tz

**Yaliyomo**

Orodha ya Majedwali ........ iii
Orodha ya Michoro ........ v
DIBAJI ........ vi
SHUKRANI ........ vii
MAANA YA VIFUPISHO ........ viii
MUHTASARI ........ x
SURA YA KWANZA ........ 1
USULI ........ 1
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Jiografia na Utawala ........ 1
1.2 Muundo wa Jeshi la Polisi Tanzania ........ 2
1.2.1 Majukumu ya Jeshi la Polisi ........ 2
1.2.2 Takwimu za Jeshi la Polisi ........ 2
1.2.3 Kitengo cha Takwimu za Jinai cha Jeshi la Polisi ........ 2
SURA YA PILI ........ 3
HALI YA UHALIFU NCHINI ........ 3
2.0 Utangulizi ........ 3
2.1 Takwimu za Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani Tanzania ........ 3
2.2 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai ........ 7
2.2.1 Makosa Dhidi ya Binadamu ........ 7
2.2.2 Makosa ya Kuwania Mali ........ 8
2.2.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii ........ 9
2.3 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai kwa Mikoa ya Kipolisi ........ 9
2.3.1 Makosa Dhidi ya Binadamu ........ 9
2.3.2 Makosa ya Kuwania Mali ........ 11
2.3.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii ........ 13
2.4 Uchambuzi wa Makosa Madogo ya Jinai kwa Mikoa ya Kipolisi ........ 15
2.5 Matukio yenye Athari Kubwa katika Jamii ........ 17
2.5.1 Mauaji na Sababu Zake ........ 17
2.5.2 Migogoro ya Ardhi ........ 19
2.5.3 Makosa ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia ........ 20
2.5.4 Makosa ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Watoto ........ 24
2.5.5 Makosa ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Watu wazima ........ 27
2.5.6 Wahamiaji Haramu ........ 30
2.5.7 Makosa ya Kimtandao ........ 32
2.5.8 Makosa ya Miamala ya Kifedha ........ 32
2.5.9 Matukio ya Kujichukulia Sheria Mkononi ........ 34
SURA YA TATU ........ 35
USALAMA BARABARANI ........ 35
3.0 Utangulizi ........ 35
3.1 Hali na Mwelekeo wa Usalama Barabarani Nchini ........ 35
3.2 Operesheni za Ukamataji wa Makosa ya Usalama Barabarani ........ 38
3.3 Ajali za Pikipiki ........ 40
3.4 Vyanzo vya Ajali za Barabarani Tanzania ........ 43

SURA YA NNE ..... 45
UHUSIANO KATI YA UHALIFU NA VIGEZO VYA KIJAMII NA KIUCHUMI ..... 45
4.0 Utangulizi ..... 45
4.1 Uhusiano wa Uhalifu na Masuala ya Kijamii na Kiuchumi ..... 45
4.2 Uhusiano wa Makosa ya Jinai, Idadi ya Watu na Eneo la Ardhi ..... 45
4.2.1 Idadi ya makosa kwa Ukubwa wa Eneo ..... 45
4.2.2 Uwiano wa Makosa kwa kila Watu 100,000 ..... 46
4.3 Matukio ya Usalama Barabarani ..... 47
SURA YA TANO ..... 49
MIKAKATI YA KUKABILIANA NA UHALIFU NA MATUKIO YA USALAMA BARABARANI ..... 49
5.0 Utangulizi ..... 49
5.1 Makosa Dhidi ya Binadamu ..... 49
5.2 Makosa ya Kuwania Mali ..... 51
5.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii ..... 52
5.4 Makosa ya Kifedha ..... 53
5.5 Makosa ya Kimtandao ..... 53
5.6 Matukio ya Ajali za Barabarani ..... 54
SURA YA SITA ..... 55
MATUKIO YALIYOVUTA HISIA KWA JAMII. ..... 55
6.0 Utangulizi ..... 55
SURA YA SABA ..... 61
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 61
7.0 Utangulizi ..... 61
7.1 Hitimisho ..... 61

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 2.1 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....4
Jedwali Na. 2.2 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa, Tanzania Bara, Januari – Juni, 2024 na 2025....5
Jedwali Na. 2.3 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania Zanzibar, Januari – Juni, 2025 ....6
Jedwali Na. 2.4 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025....7
Jedwali Na. 2.5 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Kuwania Mali kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....8
Jedwali Na. 2.6 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Kifedha kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....8
Jedwali Na. 2.7 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....9
Jedwali Na. 2.8 Idadi ya Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari - Juni, 2025....10
Jedwali Na. 2.9 Idadi ya Makosa ya Kuwania Mali kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....11
Jedwali Na. 2.10 Idadi ya Makosa ya Kifedha kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari – Juni, 2025....12
Jedwali Na. 2.11 Idadi ya Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari – Juni, 2025....14
Jedwali Na. 2.12 Idadi ya Makosa Madogo ya Jinai ya Kuwania Mali, Makosa Dhidi ya Binadamu na Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....16
Jedwali Na. 2.13 Idadi ya Makosa ya Mauaji, Waliouawa kwa Jinsi, Sababu za Kuuawa na Idadi ya Watuhumiwa kwa Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....18
Jedwali Na. 2.14 Idadi ya Migogoro ya Ardhi, Waliouawa, Waliojeruhiwa na Mali zilizoharibiwa kwa Aina ya Migogoro na Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....19
Jedwali Na. 2.15 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Makundi ya Ukatili na Aina ya Ukatili, Januari – Juni, 2025 ....21
Jedwali Na. 2.16 Idadi ya Watu Waliofanyiwa Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....22
Jedwali Na. 2.17 Idadi ya Watoto Waliofanyiwa Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....25
Jedwali Na. 2.18 Idadi ya Watu Wazima Waliofanyiwa Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....28
Jedwali Na. 2.19 Idadi ya Kesi na Wahamiaji Haramu kwa Jinsi, Utaifa na Mkoa Wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....31
Jedwali Na. 2.20 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Kimtandao kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025....32
Jedwali Na. 2.21 Idadi ya Matukio ya Uhalifu kwa Njia ya Simu na Huduma za Kifedha kwa Aina ya Tukio na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....33

Jedwali Na. 2.22 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Watu Waliouawa Kutokana na Wananchi Kujichukulia Sheria Mkononi kwa Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025 34

Jedwali Na. 3.1 Idadi ya Ajali, Vifo, Majeruhi Waliotokana na Ajali za Barabarani, Tanzania, Januari - Juni, 2025 ....36

Jedwali Na. 3.2 Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi Waliotokana na Ajali za Barabarani, Tanzania Bara, Januari – Juni, 2025 ....36

Jedwali Na. 3.3 Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi Waliotokana na Ajali za Barabarani, Tanzania Zanzibar, Januari – Juni, 2025 ....37

Jedwali Na. 3.4 Idadi ya Matukio ya Usalama Barabarani kwa Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari - Juni, 2025 ....39

Jedwali Na. 3.5 Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....40

Jedwali Na. 3.6 Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Juni, 2025....41

Jedwali Na. 3.7 Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Juni, 2025 ....41

Jedwali Na. 3.8 Idadi ya Matukio na Madhura katika Usafiri wa Pikipiki kwa Mkoa wa Kipolisi;Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....42

Jedwali Na. 3.9 Idadi ya Ajali kwa Vyanzo Vyake, Tanzania, Januari – Juni, 2025....43

Jedwali Na. 4.1 Idadi ya Makosa, Idadi ya Watu kwa kila Kosa, Makosa ya Jinai kwa kila Kilomita 100 za Mraba na Uwiano wa Makosa kwa Kila Watu 100,000 kwa Mkoa; Tanzania, Januari - Juni, 2025....47

Jedwali Na. 4.2 Idadi ya Matukio ya Usalama Barabarani, Idadi ya Watu na Askari, Uwiano wa Makosa kwa kila kilometa 100 za Mraba na Matukio kwa kila Askari kwa Mkoa;Tanzania, Januari - Juni, 2025 ....48

Jedwali Na. 5.1 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari - Juni, 2025....49

Jedwali Na. 5.2 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa ya Kuwania Mali kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....51

Jedwali Na. 5.3 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti, Kutanzua Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ....52

Jedwali Na. 5.4 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti, Kutanzua Makosa ya Kifedha kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari - Juni, 2025....53

Jedwali Na. 5.5 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa ya Kimtandao kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni 2025 ....53

Jedwali Na. 5.6 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa ya Ajali za Barabarani kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni 2025 ....54

## Orodha ya Michoro

Mchoro Na. 2.1 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025 ........ 5
Mchoro Na. 2.2 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania Bara, Januari – Juni, 2025 ........ 6
Mchoro Na. 2.3 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania Zanzibar, Januari – Juni, 2025 ........ 7
Mchoro Na. 2.4 Vyanzo vya Mauaji, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ........ 17
Mchoro Na. 3.1 Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari - Juni, 2025 ........ 36
Mchoro Na. 3.2 Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari - Juni, 2025 ........ 37
Mchoro Na. 3.3 Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari - Juni, 2025 ........ 38
Mchoro Na. 3.4 Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ........ 40
Mchoro Na. 3.5 Vyanzo vya Ajali za Barabarani, Tanzania, Januari – Juni, 2025 ........ 44

## DIBAJI

Wajibu wa Jeshi la Polisi Tanzania ni kuhakikisha kuwa amani inatawala, ulinzi wa raia na mali zao unaimarika, kunakuwepo na utulivu nchini ili kuwawezesha raia kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Matokeo yake ni kukua kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na hatimaye Taifa.



Camillus M. Wambura – IGP
Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania

Mapambano dhidi ya uhalifu ni jukumu la pamoja kati ya Jeshi la Polisi, vyombo vingine vya usalama, raia na wadau wengine ili kuweza kuushinda uhalifu wa aina zote. Kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, wahalifu wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za uhalifu na kusababisha kuibuka kwa aina mpya za uhalifu kama makosa kwa njia ya mtandao na ugaidi.

Kwa kulitambua hilo, ni wito wangu kwa kila raia wa Tanzania kushiriki katika majukumu ya ulinzi na usalama wake na jirani yake pamoja na mali zao, zikiwemo mali za umma. Kila mmoja apige vita aina yoyote ya uhalifu ili kuendelea kufanya Taifa zima kuwa salama. Nitoe wito kwa kila mwanajamii kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha uhalifu hautendeki na kama ukitendeka ahakikishe kuwa mhalifu anakamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya dola kwa wakati ili hatua stahiki za kisheria zichukuliwe. Pia kila raia kutii sheria bila shuruti ili kutolilazimu Jeshi la Polisi kumshurutisha mtu kutii sheria za nchi katika kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Nachukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuwezesha kupata ajira za kutosha na vifaa vya kufanyia kazi vilivyowezesha kupambana na uhalifu hatimae kusababisha uhalifu kupungua kulinganisha na miaka iliyopita.

Camillus M. Wambura - IGP
Mkuu wa Jeshi la Polisi
Makao Makuu ya Polisi.
Dodoma

## SHUKRANI

Taarifa hii imeandaliwa na Jeshi la Polisi nchini kupitia Kamisheni ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Namshukuru Mkuu wa Jeshi la Polisi Camillus M. Wambura (IJP) kwa maelekezo yake na kututia moyo wakati wa uandaaji wa taarifa hii. Vilevile, shukrani zangu ziende kwa watendaji wote kwa jitihada zao zilizowezesha uandaaji wa taarifa hii.



Ramadhan H. Kingai - CP
Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai

Shukurani za pekee ziende kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Dkt. Amina S. Msengwa, Kamishna Jenerali wa Magereza Jeremiah Y. Katungu na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Ndugu. Sylvester A. Mwakitalu kwa ushirikiano wao katika kufanikisha uandaaji wa taarifa hii.

Aidha, shukurani ziwaendee Maofisa, Wakaguzi, Askari wa vyeo mbalimbali na watumishi raia wa Jeshi la Polisi nchini kwa michango yao iliyofanikisha uandaaji wa taarifa hii. Kwa namna ya pekee nitoe shukrani kwa wajumbe wa kamati ya uandaaji wa taarifa hii kutoka Jeshi la Polisi nchini, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Jeshi la Magereza na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka nchini. Kamati hii inahusisha wajumbe 22 wakiongozwa na ACP Juma H. Majatta - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Takwimu Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Amani Mghamba - SSA (OTM), Valerian Tesha (NBS), Margreth Jacob (NBS), Rainer Kiama (NBS), ASP Juma Hebu (TPF), ASP Mayday Mhongole (TPF), INSP Vitalis Wantiku (TPF), INSP Elia Kuguru (TPF), A/INSP Getruda Yamsebo (TPS), WP. 2606 D/SSGT Amina Said (TPF), WP.5246 D/SGT Habiba Maganga (TPF), H.7725 D/SGT Julius Nzowa (TPF), G.3258 D/SGT John Nyemba (TPF), G.1108 D/SGT Geofrey Ipini (TPF), G.8341 D/SGT Said Samvu (TPF), G.8467 D/CPL Hemedi Sengasu (TPF), WP.9536 D/CPL Flora Loyde (TPF), H.3324 D/CPL Hamisi Mlambo (TPF), H.3627 D/CPL Soud Muhogo (TPF), J. 8194 D/C Zuberi Msenga (TPF) na J.8241 D/C Seth Maslan (TPF).



……………………………………….
Ramadhani H. Kingai – CP,
Mkurungenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai,
Makao Makuu ya Upelelezi.
Dodoma

## MAANA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| A/INSP | - | Mkaguzi Msaidizi wa Polisi/Magereza |
| ACP | - | Kamishna Msaidizi wa Polisi |
| AFRIPOL | - | Shirikisho la Majeshi ya Polisi ya Bara la Afrika |
| ASP | - | Mrakibu Msaidizi wa Polisi |
| ATM | - | Mashine zinazotumika kutoa/kuweka fedha benki |
| CP | - | Kamishna wa Polisi |
| CPA | - | Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai |
| CPF | - | Mkuu wa Jeshi la Polisi |
| D/C | - | Mpelelezi wa Cheo cha Konsitebo |
| DCEA | - | Mamlaka ya kudhibiti Dawa za Kulevya |
| DCI | - | Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai |
| D/CPL | - | Mpelelezi wa Cheo cha Koplo |
| D/SGT | - | Mpelelezi wa Cheo cha Sajenti |
| D/SSGT | - | Mpelelezi wa Cheo cha Stafu Sajenti |
| DPP | - | Mkurugenzi wa Mashtaka |
| EAPCCO | - | Shirikisho la Wakuu wa Polisi Mashariki Mwa Afrika |
| IGP | - | Mkuu wa Jeshi la Polisi |
| INSP | - | Mkaguzi wa Polisi/Magereza |
| INTERPOL | - | Shirikisho la Kimataifa la Polisi |
| IOM | - | Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji |
| K/f | - | Kifungu |
| LATRA | - | Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Tanzania |
| NBS | - | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| NFA | - | Hakuna hatua inayoendelea |
| NGO'S | - | Mashirika yasiyo ya Kiserikali |
| NOD | - | Hakuna kosa lililobainika |
| NPSA | - | Sheria ya Huduma ya Taifa ya Mashtaka |
| OC CID | - | Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya |
| OTM | - | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka |
| PGO | - | Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi |
| PSV | - | Magari yaliyoruhusiwa na Serikali kubeba abiria |
| RCO | - | Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa |
| RPC | - | Kamanda wa Polisi wa Mkoa |
| RTO | - | Mkuu wa Usalama Barabarani wa Mkoa |
| SAR | - | Silaha Ndogo ya Kivita |
| SARPCCO | - | Shirikisho la Jumuiya ya Majeshi ya Polisi ya Nchi za Kusini Mwa Afrika |
| SMG | - | Silaha ya Kivita |
| SSA | - | Wakili wa Serikali Mwandamizi |

| | | |
|---|---|---|
| TAKUKURU | - | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TANAPA | - | Shirika la Hifadhi za Taifa |
| TAZARA | - | Tanzania Zambia Railway Authority |
| TAWA | - | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TPF | - | Jeshi la Polisi Tanzania |
| TPS | - | Jeshi la Magereza Tanzania |
| TZS | - | Shilingi ya Tanzania |
| “U” | - | Hakuna mtuhumiwa aliyekamatwa |
| VTS | - | Mfumo wa Ufuataliaji wa Mwendokasi wa Magari |
| ZCO | - | Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda Maalum |

## MUHTASARI

Taarifa ya hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 imezingatia kwa ujumla matukio yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini kwa kipindi hicho. Makosa ya Jinai na Matukio ya Usalama barabarani yamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni makubwa na madogo. Aidha, makosa ya jinai yamegawanywa katika makundi matatu; makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii.

Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, jumla ya makosa 1,653,358 ya jinai na Usalama barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi nchini yakilinganishwa na matukio 1,847,551 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 194,193 sawa na asilimia 10.5.

Kwa upande wa makosa ya jinai, kumekuwa na upungufu wa makosa 9,971 sawa na asilimia 3.3 kutoka makosa 303,861 yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2024, ikilinganishwa na makosa 293,890 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2025. Katika makosa yote ya jinai yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, makosa makubwa yalikuwa 22,920 na madogo 270,970 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2024`ambapo makosa makubwa yalikuwa 25,968 na madogo 277,893. Huu ni upungufu wa makosa makubwa 3,048 sawa na asilimia 11.7 na upungufu wa makosa madogo 6,923 sawa na asilimia 2.5.

Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 matukio ya Usalama barabarani yaliyoripotiwa yalikuwa 1,359,468 ikilinganishwa na matukio 1,543,690 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 184,222 sawa na asilimia 11.9. Katika matukio yote ya Usalama barabarani, matukio makubwa (ajali) yalikuwa 642 na matukio madogo yalikuwa 1,358,826 ikilinganishwa na matukio makubwa 886 na matukio madogo 1,542,804 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024, huu ni upungufu wa matukio makubwa 244 sawa na asilimia 27.5 na upungufu wa matukio madogo 183,978 sawa na asilimia 11.9.

Aidha katika matukio makubwa yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 watu 640 walipoteza maisha na watu 1,100 walijeruhiwa ikilinganishwa na watu 827 waliopoteza maisha na watu 1,235 waliojeruhiwa kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa vifo 187 (asilimia 22.6) na upungufu wa majeruhi 135 (asilimia 10.9). Kati ya Matukio makubwa 642 ya ajali za barabarani, ajali za pikipiki zilizoripotiwa zilikuwa 144 ikilinganishwa na ajali 259 zilizoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 115 sawa na asilimia 44.4.

Hata hivyo, jamii iliendelea kushuhudia vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile kubaka, kulawiti, kutupa watoto, wizi wa watoto na kukeketa. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 jumla ya Madhura 15,068 walifanyiwa ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikilinganishwa na Madhura 19,537 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa Madhura 4,469 sawa na asilimia 22.9.

# SURA YA KWANZA

# USULI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia jiografia ya nchi na majukumu ya msingi ya Jeshi la Polisi Tanzania. Takwimu za hali ya uhalifu nchini zinalisaidia Jeshi la Polisi katika kupanga mipango na programu za muda mfupi, kati na mrefu ili kudhibiti hali ya uhalifu nchini na kuendeleza hali ya amani na utulivu iliyopo ambayo ni muhimu katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

### 1.1 Jiografia na Utawala

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muungano wa nchi mbili huru za Tanganyika na Zanzibar ulioundwa tarehe 26 Aprili 1964. Tanzania ipo kati ya Latitudo $1^0$ na $12^0$ Kusini mwa Ikweta; na kati ya Longitudo $29^0$ na $41^0$ Mashariki mwa Greenwich. Tanzania ina eneo la ardhi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 945,500 na eneo lenye maji ni kilomita za mraba 61,500. Kwa upande wa Kaskazini imepakana na nchi za Kenya na Uganda; Magharibi imepakana na nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; Kusini imepakana na nchi za Malawi, Zambia na Msumbiji; na Mashariki imepakana na Bahari ya Hindi.

Tanzania ina maziwa makuu matatu ambayo ni Victoria, Tanganyika na Nyasa. Tanzania ina vivutio vingi vya kitalii ikiwemo mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote Afrika na wenye theluji kwa kipindi chote cha mwaka. Vivutio vingine ni pamoja na mbuga za wanyama, mambo ya kale na fukwe nzuri za bahari katika Pwani ya Tanzania Bara na visiwa vya Tanzania Zanzibar, yaani Unguja na Pemba.

Tanzania ina hali ya hewa ya kitropiki yenye misimu miwili ya mvua ya masika na vuli katika sehemu kubwa ya nchi. Shughuli kuu za uchumi ni kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini, utalii, viwanda na utoaji huduma za kijamii. Kulingana na makadirio ya idadi ya watu kwa mwaka 2024 Tanzania ina jumla ya watu 66,278,276 (wanaume 32,478,878 na wanawake 33,799,398). Licha ya kuwa Tanzania ina makabila yanayozidi 120, lugha kuu ya Taifa ni Kiswahili kinachozungumzwa takribani na watu wote nchini.

Tanzania ni nchi inayofuata demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Dola ya Tanzania ina mihimili mitatu - Bunge, Mahakama na Serikali. Mhimili wa serikali umeundwa kwa mfumo wa serikali mbili, ambazo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshaongozwa na Marais sita na ile ya Zanzibar imeshaongozwa na Marais wanane. Kiutawala, Tanzania imegawanyika katika mikoa 31; mikoa 26 Tanzania Bara na mikoa mitano (5) Zanzibar.

## 1.2 Muundo wa Jeshi la Polisi Tanzania

Jeshi la Polisi limeanzishwa kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara ya 147 (4) na Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 Kifungu cha 3 kama ilivyoboreshwa mwaka 2023. Pamoja na kuzingatia sheria na katiba ya nchi, pia Jeshi la Polisi huongozwa kwa kuzingatia kanuni za kudumu za Jeshi (PGO), zenye misingi (vithaminiwa) ya ujasiri, uwazi, utiifu, ukweli, uadilifu, uaminifu, haki na kuheshimiana. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, Jeshi la Polisi huzingatia mikataba ya kimataifa ya kiusalama na haki za binadamu.

Muundo wa Jeshi la Polisi umegawanyika katika Kamisheni nane (8) za kiutendaji, ambazo ni Kamisheni ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimali watu; Kamisheni ya Fedha na Lojistiki; Kamisheni ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai; Kamisheni ya Operesheni na Mafunzo; Kamisheni ya Ushirikishwaji wa Jamii; Kamisheni ya Intelijensia ya Jinai; Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi na Kamisheni ya Zanzibar.

Kiutendaji, Jeshi la Polisi lina mikoa ya kipolisi 35, mikoa 30 Tanzania Bara, mikoa mitano (5) Tanzania Zanzibar na vikosi 12.

### 1.2.1 Majukumu ya Jeshi la Polisi

Majukumu ya Jeshi la Polisi yameainishwa katika Kifungu cha 5 (1) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 kama ilivyoboreshwa mwaka 2023. Majukumu hayo ni pamoja na kulinda amani, kulinda usalama wa raia na mali zao, kuzuia makosa kabla hayajatendeka, upelelezi wa makosa ya jinai, kuwakamata wahalifu na kuwafikisha Mahakamani na kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za nchi.

### 1.2.2 Takwimu za Jeshi la Polisi

Jeshi la Polisi lina Takwimu za aina mbili, Takwimu za kiutawala na takwimu za uhalifu. Takwimu za kiutawala zinajumuisha rasilimali watu, vifaa na fedha. Takwimu za uhalifu zinajumuisha makosa ya jinai na matukio ya usalama barabarani yanayoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini. Takwimu hizi huliwezesha Jeshi la Polisi kujua hali ya uhalifu nchini; kupanga mipango yake ya kiutendaji; na kubuni mbinu mbalimbali za kuzuia na kupambana na uhalifu na wahalifu nchini.

### 1.2.3 Kitengo cha Takwimu za Jinai cha Jeshi la Polisi

Kitengo cha takwimu za jinai kipo chini ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), kwa mujibu wa PGO 6 (f) ikisomwa pamoja na PGO 41. Kitengo hiki kimepewa majukumu ya kukusanya taarifa zote za uhalifu zinazoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini na kuzifanyia kazi kwa kuzichakata, kuzichambua, kuzihifadhi na kuandaa taarifa ya hali ya uhalifu nchini kwa kipindi cha robo mwaka, nusu mwaka na kwa mwaka mzima. Kazi hii hufanywa kwa kushirikiana na vitengo vingine ndani ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufikia malengo ya Jeshi la Polisi na wadau wengine.

# SURA YA PILI

# HALI YA UHALIFU NCHINI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaonesha kwa ujumla matukio mbalimbali ya uhalifu yaliyoripotiwa nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025. Matukio hayo yamegawanywa katika sehemu kuu mbili ambazo ni Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani.

a. Makosa ya Jinai

Makosa ya Jinai yamegawanyika katika sehemu kuu mbili, makosa makubwa na makosa madogo.

i. Makosa makubwa ya jinai: ni yale ambayo yamepewa kipaumbele na Jeshi la Polisi katika kuyashughulikia na mengi ya makosa haya yana madhara makubwa ambayo huonekana moja kwa moja katika jamii. Mfano wa makosa hayo ni mauaji, unyang’anyi wa aina zote na kupatikana na dawa za kulevya.

ii. Makosa madogo ya jinai; ni yale ambayo yanapotendeka hayana madhara makubwa katika jamii mfano wa makosa hayo ni wizi kutoka maungoni, shambulio la kawaida na lugha ya matusi.

b. Matukio ya Usalama Barabarani

i. Matukio ya usalama barabarani yamegawanyika katika sehemu mbili, matukio makubwa na matukio madogo. Matukio makubwa ya usalama barabarani: ni ajali za barabarani zinazosababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na miundombinu.

ii. Makosa madogo ya usalama barabarani: ni makosa ambayo yakifanyika hayaleti madhara kwa wakati huo kama vile kuendesha vyombo vya moto bila leseni ya udereva na vibali vingine, kuegesha chombo bila kufuata utaratibu, kwenda mwendokasi, kutozingatia miongozo ya taa za barabarani na kutofunga mkanda.

Pamoja na makosa hayo kutokuleta madhara kwa wakati huo, makosa hayo huweza kuwa vyanzo vya ajali kama hayakuzingatiwa. Mtuhumiwa anapokamatwa na kupatikana na hatia hupewa adhabu ya kifungo, kutozwa faini au kupewa onyo.

## 2.1 Takwimu za Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani Tanzania

Sehemu hii inaonesha takwimu za hali ya uhalifu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 zikilinganishwa na takwimu za kipindi kama hicho mwaka 2024. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, jumla ya matukio 1,653,358 ya jinai na usalama barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi

nchini ikilinganishwa na matukio 1,847,551 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 194,193 sawa na asilimia 10.5.

Takwimu zinaonesha jumla ya makosa makubwa na madogo ya jinai 293,890 yaliripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 ikilinganishwa na makosa 303,861 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka, 2024. Huu ni upungufu wa makosa 9,971 sawa na asilimia 3.3.

Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, makosa makubwa ya jinai yalikuwa 22,920 ikilinganishwa na makosa 25,968 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 3,048 sawa na asilimia 11.7.

Makosa madogo ya jinai yalikuwa 270,970 katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 ikilinganishwa na makosa 277,893 kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 6,923 sawa na asilimia 2.5.

Aidha, jumla ya matukio makubwa na madogo ya Usalama barabarani yalikuwa 1,359,468 katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, ikilinganishwa na matukio 1,543,690 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 184,222 sawa na asilimia 11.9.

Matukio makubwa ya usalama barabarani yalikuwa 642 katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 ikilinganishwa na matukio 886 kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 244 sawa na asilimia 27.5

Matukio madogo ya usalama barabarani yalikuwa 1,358,826 katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 ikilinganishwa na matukio 1,542,804 ya kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 183,978 sawa na asilimia 11.9.

**Jedwali Na. 2.1 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Aina ya Makosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| **Jinai** | | | | |
| Madogo | 277,893 | 270,970 | -6,923 | -2.5 |
| Makubwa | 25,968 | 22,920 | -3,048 | -11.7 |
| **Jumla Ndogo** | **303,861** | **293,890** | **-9,971** | **-3.3** |
| **Usalama Barabarani** | | | | |
| Madogo | 1,542,804 | 1,358,826 | -183,978 | -11.9 |
| Makubwa | 886 | 642 | -244 | -27.5 |
| **Jumla Ndogo** | **1,543,690** | **1,359,468** | **-184,222** | **-11.9** |
| **Jumla Kuu** | **1,847,551** | **1,653,358** | **-194,193** | **-10.5** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 2.1 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025**




Jedwali Na.2.2 na Mchoro Na.2.2 yanaonesha mchanganuo wa makosa ya jinai na matukio ya usalama barabarani Tanzania Bara. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, jumla ya matukio 1,613,639 ya Jinai na Usalama barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi Tanzania Bara ikilinganishwa na matukio 1,818,041 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa matukio 204,402 sawa na asilimia 11.2. Makosa ya jinai Tanzania Bara yamepungua kwa makosa 8,325 kutoka makosa 291,422 yaliyoripotiwa mwaka 2024 hadi makosa 283,097 mwaka 2025 sawa na asilimia 2.9. Matukio ya usalama barabarani yamepungua kwa matukio 196,077 kutoka matukio 1,526,619 hadi matukio 1,330,542 mwaka 2025 sawa na asilimia 12.8.

**Jedwali Na. 2.2 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa, Tanzania Bara, Januari – Juni, 2024 na 2025**

| Aina ya Makosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| **Jinai** | | | | |
| Madogo | 267,102 | 261,385 | -5,717 | -2.1 |
| Makubwa | 24,320 | 21,712 | -2,608 | -10.7 |
| **Jumla Ndogo** | **291,422** | **283,097** | **-8,325** | **-2.9** |
| **Usalama Barabarani** | | | | |
| Madogo | 1,525,846 | 1,330,000 | -195,846 | -12.8 |
| Makubwa | 773 | 542 | -231 | -29.8 |
| **Jumla Ndogo** | **1,526,619** | **1,330,542** | -196,077 | **-12.8** |
| **Jumla Kuu** | **1,818,041** | **1,613,639** | **204,402** | **-11.2** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

**Mchoro Na. 2.2 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania Bara, Januari – Juni, 2025**




Jedwali Na. 2.3 na Mchoro Na. 2.3 yanaonesha mchanganuo wa makosa ya jinai na matukio ya usalama barabarani Tanzania Zanzibar. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, jumla ya matukio 39,719 ya jinai na Usalama barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi Tanzania Zanzibar ikilinganishwa na matukio 29,510 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Hili ni ongezeko la matukio 10,209 sawa na asilimia 34.6.

Makosa ya jinai yamepungua kwa makosa 1,646 kutoka makosa 12,439 mwaka 2024 hadi makosa 10,793 mwaka 2025 sawa na asilimia 13.2. Matukio ya usalama barabarani yameongezeka kwa matukio 11,855 kutoka matukio 17,071 mwaka 2024 hadi matukio 28,926 mwaka 2025 sawa na asilimia 69.4.

**Jedwali Na. 2.3 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania Zanzibar, Januari – Juni, 2025**

| Aina ya Makosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| **Jinai** | | | | |
| Madogo | 10,791 | 9,585 | -1,206 | -11.2 |
| Makubwa | 1,648 | 1,208 | -440 | -26.7 |
| **Jumla Ndogo** | **12,439** | **10,793** | **-1,646** | **-13.2** |
| **Usalama Barabarani** | | | | |
| Madogo | 16,958 | 28,826 | 11,868 | 70.0 |
| Makubwa | 113 | 100 | -13 | -11.5 |
| **Jumla Ndogo** | **17,071** | **28,926** | **11,855** | **69.4** |
| **Jumla Kuu** | **29,510** | **39,719** | **10,209** | **34.6** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 2.3 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani kwa Aina ya Makosa; Tanzania Zanzibar, Januari – Juni, 2025**




## 2.2 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai

Makosa makubwa ya jinai ni pamoja na makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Uchambuzi umefanyika kwa aina ya makosa yaliyoripotiwa katika kila kundi.

### 2.2.1 Makosa Dhidi ya Binadamu

Baadhi ya makosa yaliyopo katika kundi hili ni mauaji, kubaka, kulawiti na usafirishaji haramu wa binadamu. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, jumla ya makosa 5,988 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 6,542 kwa mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 554 sawa na asilimia 8.5. Upungufu wa makosa katika kundi hili unatokana na kupungua kwa makosa ya Kubaka (393), Mauaji (170) na kutupa watoto (10). (Jedwali Na. 2.4).

**Jedwali Na. 2.4 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Aina ya Kosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Mauaji | 1,096 | 926 | -170 | -15.5 |
| Kubaka | 4,331 | 3,938 | -393 | -9.1 |
| Kulawiti | 988 | 997 | 9 | 0.9 |
| Wizi wa Watoto | 31 | 44 | 13 | 41.9 |
| Kutupa Watoto | 90 | 80 | -10 | -11.1 |
| Usafirishaji Haramu wa Binadamu | 6 | 3 | -3 | -50.0 |
| **Jumla** | **6,542** | **5,988** | **-554** | **-8.5** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

### 2.2.2 Makosa ya Kuwania Mali

Makosa yaliyopo katika kundi hili yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni makosa yanayohusu vitu na makosa yanayohusu fedha (makosa ya kifedha). Baadhi ya makosa yanayohusu vitu ni unyang'anyi, uvunjaji na wizi. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, jumla ya makosa 9,030 yanayohusu vitu yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 10,817 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 1,787 sawa na asilimia 16.5. Makosa yaliyopungua kwa idadi kubwa kwenye kundi hili ni Uvunjaji (1,621), unyang'anyi wa kutumia nguvu (301) na unyang'anyi wa kutumia silaha (93), (Jedwali Na. 2.5).

**Jedwali Na. 2.5 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Kuwania Mali kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Aina ya Kosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Wizi wa silaha | 11 | 6 | -5 | -45.5 |
| Unyang'anyi wa k/silaha | 220 | 127 | -93 | -42.3 |
| Unyang'anyi wa k/nguvu | 579 | 278 | -301 | -52.0 |
| Uvunjaji | 5,848 | 4,227 | -1,621 | -27.7 |
| Wizi | 185 | 236 | 51 | 27.6 |
| Wizi wa pikipiki | 1,984 | 2,003 | 19 | 1.0 |
| Wizi wa magari | 36 | 29 | -7 | -19.4 |
| Wizi wa mifugo | 1,670 | 1,749 | 79 | 4.7 |
| Kuharibu miundombinu | 29 | 120 | 91 | 313.8 |
| Kuchoma nyumba moto | 255 | 255 | 0 | 0.0 |
| **Jumla** | **10,817** | **9,030** | **-1,787** | **-16.5** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

#### 2.2.2.1 Makosa ya Kifedha

Makosa ya kifedha ni kitendo chochote cha uvunjaji wa sheria ambacho kinahusisha kuchukua, kudhibiti au kutumia fedha, mali au rasilimali nyingine kwa njia isiyo halali. Mara nyingi hutumia udanganyifu, hila au matumizi mabaya ya uaminifu kwa mtu binafsi, Taasisi au Serikali. Baadhi ya makosa yaliyopo katika kundi hili ni kughushi, noti bandia, wizi katika mabenki, Serikali kuu/mitaa na vyama vya siasa. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, jumla ya makosa 457 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 489 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 32 sawa na asilimia 6.5. Makosa yaliyoripotiwa kwa idadi kubwa ni kughushi (352), noti bandia (77) na wizi katika mashirika ya umma (16), (Jedwali Na.2.6).

**Jedwali Na. 2.6 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa ya Kifedha kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Aina ya Kosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Noti Bandia | 69 | 77 | 8 | 11.6 |
| Wizi K/ Mabenki | 0 | 2 | 2 | 0.0 |
| Wizi K/ Mashirika ya Umma | 20 | 16 | -4 | -20.0 |
| Wizi K/ Vyama vya Ushirika | 1 | 1 | 0 | 0.0 |
| Wizi K/ Serikali za Mitaa | 7 | 4 | -3 | -42.9 |
| Wizi K/ Serikali Kuu | 16 | 4 | -12 | -75.0 |
| Wizi K/ Vyama vya Siasa | 0 | 1 | 1 | 0.0 |
| Kughushi | 376 | 352 | -24 | -6.4 |
| **Jumla** | **489** | **457** | **-32** | **-6.5** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

### 2.2.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii

Baadhi ya makosa yaliyopo katika kundi hili ni kupatikana na dawa za kulevya, nyara za serikali, silaha na wahamiaji haramu. Jumla ya makosa 7,445 yaliripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 ikilinganishwa na makosa 8,121 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Huu ni upungufu wa makosa 676 sawa na asilimia 8.3.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kudhibiti makosa yaliyomo katika kundi hili kwa sehemu kubwa yanatokana na juhudi za Jeshi la Polisi katika kufanya doria, kutoa elimu kwa jamii na kufanya misako kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi kwa ujumla (Jedwali Na. 2.7).

**Jedwali Na. 2.7 Idadi, Tofauti na Badiliko (Asilimia) la Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Aina ya Kosa | 2024 | 2025 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Kupatikana na silaha | 94 | 104 | 10 | 10.6 |
| Dawa za kulevya za viwandani | 73 | 14 | -59 | -80.8 |
| Kupatikana na bhangi | 3,172 | 2,881 | -291 | -9.2 |
| Kupatikana na mashamba ya bhangi | 10 | 23 | 13 | 130.0 |
| Kupatikana na mirungi | 669 | 657 | -12 | -1.8 |
| Kupatikana na nyara za serikali | 295 | 353 | 58 | 19.7 |
| Magendo | 94 | 73 | -21 | -22.3 |
| Rushwa | 1 | 0 | -1 | -100.0 |
| Kupatikana na pombe ya moshi | 2,621 | 2,433 | -188 | -7.2 |
| Kupatikana na mitambo ya pombe ya moshi | 188 | 134 | -54 | -28.7 |
| Kupatikana na risasi | 5 | 10 | 5 | 100.0 |
| Uvuvi haramu | 125 | 193 | 68 | 54.4 |
| Kupatikana mazao ya misitu | 164 | 121 | -43 | -26.2 |
| Kupatikana na madini | 3 | 22 | 19 | 633.3 |
| Kupatikana mazao ya bahari | 2 | 9 | 7 | 350.0 |
| Wahamiaji haramu | 605 | 418 | -187 | -30.9 |
| **Jumla** | **8,121** | **7,445** | **-676** | **8.3** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

## 2.3 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai kwa Mikoa ya Kipolisi

Makosa makubwa ya jinai yametenganishwa kimikoa kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Takwimu zinaonesha tofauti ya makosa kimkoa kutokana na kundi na idadi ya makosa yaliyoripotiwa.

### 2.3.1 Makosa Dhidi ya Binadamu

Mikoa ya kipolisi iliyoripoti makosa dhidi ya binadamu kwa idadi kubwa katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025 Tanzania Bara ni Kinondoni (377), Dodoma (338), Tanga (298), Morogoro (264) na Ilala (254). Mikoa yenye idadi ndogo ya makosa ni Simiyu (70), Geita (75), Katavi (82), Lindi (88) na Rukwa (102).

Mikoa ya kipolisi iliyoripoti makosa dhidi ya binadamu kwa idadi kubwa Tanzania Zanzibar ni Mjini Magharibi (227) na Kusini Unguja (63). Mikoa yenye idadi ndogo ya makosa ni Kusini Pemba (33) na Kaskazini Pemba (40). Makosa yaliyoripotiwa katika kundi hili kwa idadi kubwa Tanzania Bara na Zanzibar ni kubaka (3,938), kulawiti (997) na mauaji (926), (Jedwali Na. 2.8)

**Jedwali Na. 2.8 Idadi ya Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari - Juni, 2025**

| Mkoa | Mauaji | Kubaka | Kutupa watoto | Kulawiti | Wizi wa watoto | Usafirishaji binadamu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 29 | 135 | 4 | 65 | 1 | 0 | 234 |
| Ilala | 10 | 164 | 11 | 68 | 1 | 0 | 254 |
| Temeke | 10 | 181 | 3 | 47 | 5 | 0 | 246 |
| Kinondoni | 19 | 239 | 9 | 107 | 3 | 0 | 377 |
| Dodoma | 52 | 211 | 2 | 70 | 1 | 2 | 338 |
| Geita | 30 | 35 | 0 | 7 | 3 | 0 | 75 |
| Iringa | 56 | 151 | 1 | 32 | 2 | 0 | 242 |
| Kagera | 61 | 150 | 7 | 12 | 4 | 0 | 234 |
| Katavi | 28 | 48 | 0 | 6 | 0 | 0 | 82 |
| Kigoma | 35 | 117 | 1 | 44 | 1 | 0 | 198 |
| Kilimanjaro | 19 | 127 | 7 | 53 | 0 | 0 | 206 |
| Lindi | 14 | 58 | 1 | 15 | 0 | 0 | 88 |
| Mara | 27 | 111 | 1 | 19 | 5 | 0 | 163 |
| Manyara | 31 | 105 | 2 | 31 | 0 | 0 | 169 |
| Mbeya | 45 | 169 | 7 | 30 | 2 | 0 | 253 |
| Morogoro | 48 | 159 | 6 | 48 | 3 | 0 | 264 |
| Mtwara | 19 | 97 | 3 | 25 | 0 | 0 | 144 |
| Mwanza | 36 | 135 | 3 | 26 | 0 | 0 | 200 |
| Njombe | 25 | 85 | 0 | 18 | 2 | 0 | 130 |
| Pwani | 26 | 149 | 2 | 29 | 1 | 0 | 207 |
| Rufiji | 8 | 155 | 0 | 15 | 0 | 0 | 178 |
| Rukwa | 23 | 67 | 2 | 10 | 0 | 0 | 102 |
| Ruvuma | 30 | 67 | 0 | 14 | 0 | 0 | 111 |
| Shinyanga | 30 | 100 | 0 | 15 | 4 | 0 | 149 |
| Simiyu | 16 | 51 | 0 | 1 | 1 | 1 | 70 |
| Singida | 36 | 47 | 0 | 23 | 0 | 0 | 106 |
| Songwe | 36 | 87 | 4 | 17 | 1 | 0 | 145 |
| Tabora | 29 | 103 | 1 | 39 | 1 | 0 | 173 |
| Tanga | 33 | 222 | 0 | 43 | 0 | 0 | 298 |
| Tarime - Rorya | 38 | 75 | 1 | 12 | 2 | 0 | 128 |
| Wanamaji | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Reli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| TAZARA | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Viwanja vya Ndege | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Bandari | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Tanzania Bara** | **900** | **3,600** | **78** | **941** | **43** | **3** | **5,565** |
| Kaskazini Pemba | 0 | 36 | 0 | 4 | 0 | 0 | 40 |
| Kaskazini Unguja | 5 | 51 | 0 | 4 | 0 | 0 | 60 |
| Kusini Pemba | 2 | 25 | 0 | 6 | 0 | 0 | 33 |
| Kusini Unguja | 5 | 55 | 2 | 1 | 0 | 0 | 63 |
| Mjini Magharibi | 14 | 171 | 0 | 41 | 1 | 0 | 227 |
| **Tanzania Zanzibar** | **26** | **338** | **2** | **56** | **1** | **0** | **423** |
| **Jumla** | **926** | **3,938** | **80** | **997** | **44** | **3** | **5,988** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

### 2.3.2 Makosa ya Kuwania Mali

Mikoa ya kipolisi iliyoripoti makosa ya kuwania mali kwa idadi kubwa katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025 Tanzania Bara ni Kinondoni (895), Morogoro (533), Dodoma, Kagera (501 kila mmoja) na Tanga (500). Mikoa yenye idadi ndogo ya makosa ni Geita (43), Shinyanga (46), Katavi (61), Singida na Simiyu (90 kila mmoja).

Mikoa ya kipolisi iliyoripoti makosa ya kuwania mali kwa idadi kubwa Tanzania Zanzibar ni Mjini Magharibi (268) na Kusini Unguja (192). Mikoa yenye idadi ndogo ya makosa ni Kaskazini Pemba (80) na Kaskazini Unguja (90). Makosa yaliyoripotiwa katika kundi hili kwa idadi kubwa Tanzania Bara na Zanzibar ni Uvunjaji (4,227), Wizi wa Pikipiki (2,003) na Wizi wa Mifugo (1,749). (Jedwali Na. 2.9).

**Jedwali Na. 2.9 Idadi ya Makosa ya Kuwania Mali kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi; Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Mkoa | Wizi wa Silaha | Unyang'anyi wa Kutumia Silaha | Unyang'anyi wa Kutumia Nguvu | Uvunjaji | Wizi wa Pikipiki | Wizi wa Magari | Wizi | Wizi wa Mifugo | Kuharibu Miundombinu | Kuchoma Nyumba Moto | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 0 | 4 | 7 | 355 | 37 | 0 | 5 | 51 | 1 | 4 | 464 |
| Ilala | 0 | 3 | 12 | 174 | 222 | 10 | 20 | 14 | 10 | 6 | 471 |
| Temeke | 0 | 4 | 5 | 149 | 147 | 1 | 8 | 9 | 1 | 3 | 327 |
| Kinondoni | 0 | 27 | 13 | 469 | 287 | 5 | 8 | 65 | 9 | 12 | 895 |
| Dodoma | 0 | 7 | 9 | 239 | 98 | 2 | 0 | 131 | 10 | 5 | 501 |
| Geita | 0 | 9 | 3 | 12 | 10 | 2 | 3 | 2 | 1 | 1 | 43 |
| Iringa | 1 | 1 | 11 | 61 | 18 | 0 | 9 | 33 | 0 | 2 | 136 |
| Kagera | 0 | 2 | 11 | 187 | 112 | 4 | 9 | 146 | 4 | 26 | 501 |
| Katavi | 0 | 0 | 1 | 17 | 13 | 0 | 0 | 30 | 0 | 0 | 61 |
| Kigoma | 0 | 3 | 8 | 49 | 26 | 0 | 6 | 23 | 1 | 11 | 127 |
| Kilimanjaro | 0 | 0 | 5 | 25 | 79 | 0 | 64 | 35 | 6 | 11 | 225 |
| Lindi | 0 | 1 | 2 | 84 | 32 | 0 | 1 | 16 | 0 | 4 | 140 |
| Mara | 0 | 2 | 4 | 39 | 22 | 0 | 1 | 42 | 8 | 10 | 128 |
| Manyara | 0 | 3 | 12 | 138 | 30 | 1 | 0 | 32 | 7 | 6 | 229 |
| Mbeya | 1 | 2 | 29 | 157 | 29 | 2 | 2 | 93 | 1 | 4 | 320 |
| Morogoro | 1 | 2 | 17 | 310 | 105 | 2 | 11 | 66 | 9 | 10 | 533 |
| Mtwara | 0 | 0 | 3 | 139 | 25 | 0 | 7 | 17 | 5 | 14 | 210 |
| Mwanza | 0 | 3 | 11 | 103 | 34 | 0 | 8 | 47 | 2 | 4 | 212 |
| Njombe | 1 | 1 | 2 | 38 | 94 | 0 | 2 | 29 | 0 | 4 | 171 |
| Pwani | 0 | 17 | 2 | 47 | 49 | 0 | 3 | 103 | 7 | 15 | 243 |
| Rufiji | 0 | 6 | 17 | 275 | 13 | 0 | 0 | 43 | 0 | 5 | 359 |
| Rukwa | 0 | 0 | 0 | 135 | 25 | 0 | 1 | 61 | 2 | 3 | 227 |
| Ruvuma | 0 | 1 | 1 | 49 | 103 | 0 | 9 | 68 | 4 | 14 | 249 |
| Shinyanga | 0 | 1 | 2 | 30 | 6 | 0 | 0 | 4 | 2 | 1 | 46 |
| Simiyu | 1 | 3 | 0 | 20 | 37 | 0 | 6 | 16 | 3 | 4 | 90 |
| Singida | 1 | 3 | 2 | 54 | 13 | 0 | 4 | 12 | 1 | 0 | 90 |
| Songwe | 0 | 1 | 4 | 102 | 28 | 0 | 1 | 25 | 4 | 4 | 169 |
| Tabora | 0 | 3 | 31 | 190 | 39 | 0 | 14 | 79 | 3 | 15 | 374 |
| Tanga | 0 | 7 | 9 | 193 | 58 | 0 | 1 | 193 | 6 | 33 | 500 |
| Tarime – Rorya | 0 | 1 | 15 | 100 | 29 | 0 | 3 | 69 | 4 | 8 | 229 |
| Wanamaji | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Reli | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 8 | 0 | 11 |
| TAZARA | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Viwanja vya Ndege | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Bandari | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Tanzania Bara** | **6** | **117** | **250** | **3,944** | **1,820** | **29** | **213** | **1,554** | **119** | **239** | **8,291** |
| Kaskazini Pemba | 0 | 2 | 1 | 51 | 1 | 0 | 1 | 23 | 0 | 1 | 80 |
| Kaskazini Unguja | 0 | 0 | 3 | 55 | 4 | 0 | 8 | 18 | 0 | 2 | 90 |
| Kusini Pemba | 0 | 6 | 3 | 64 | 6 | 0 | 0 | 27 | 0 | 3 | 109 |
| Kusini Unguja | 0 | 2 | 2 | 45 | 57 | 0 | 12 | 70 | 0 | 4 | 192 |
| Mjini Magharibi | 0 | 0 | 19 | 68 | 115 | 0 | 2 | 57 | 1 | 6 | 268 |
| **Tanzania Zanzibar** | **0** | **10** | **28** | **283** | **183** | **0** | **23** | **195** | **1** | **16** | **739** |
| **Tanzania** | **6** | **127** | **278** | **4,227** | **2,003** | **29** | **236** | **1,749** | **120** | **255** | **9,030** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

### 2.3.2.1 Makosa ya Kifedha

Mikoa ya kipolisi iliyoripoti makosa ya kifedha kwa idadi kubwa katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025 Tanzania bara ni Kinondoni (89), Ilala (67), Dodoma (39), Mwanza (29) na Arusha (27). Mikoa yenye idadi ndogo ya makosa ni Rukwa, Rufiji, Lindi (2 kila mmoja), Tarime Rorya na Singida (3 kila mmoja).

Mkoa wa kipolisi ulioripoti makosa ya kifedha kwa idadi kubwa Tanzania Zanzibar ni Mjini Magharibi (12) na idadi ndogo ya makosa ni Kusini Pemba na Kusini Unguja (1 kila mmoja). Makosa yaliyoripotiwa katika kundi hili kwa idadi kubwa Tanzania Bara na Zanzibar ni Kughushi (352), Noti Bandia (77) na Wizi katika Mashirika ya Umma (16), (Jedwali Na. 2.10).

**Jedwali Na. 2.10 Idadi ya Makosa ya Kifedha kwa Aina ya Kosa na Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Mkoa | Noti Bandia | Wizi katika: Benki | Wizi katika: Mashirika ya Umma | Wizi katika: Vyama vya ushirika | Wizi katika: Serikali za mitaa | Wizi katika: Serikali kuu | Wizi katika: Vyama vya siasa | Kughushi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 18 | 27 |
| Ilala | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 56 | 67 |
| Temeke | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 18 |
| Kinondoni | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 77 | 89 |
| Dodoma | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 39 |
| Geita | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Iringa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 6 |
| Kagera | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 10 |
| Katavi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kigoma | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 6 | 7 |
| Kilimanjaro | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 18 | 23 |
| Lindi | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Mara | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 10 |
| Manyara | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 13 |
| Mbeya | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 12 |
| Morogoro | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 5 |
| Mtwara | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 |
| Mwanza | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 | 29 |
| Njombe | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Pwani | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 13 |
| Rufiji | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Rukwa | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Ruvuma | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 |
| Shinyanga | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 7 |
| Simiyu | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 8 |
| Singida | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Songwe | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 6 |
| Tabora | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 8 |
| Tanga | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 7 | 9 |
| Tarime – Rorya | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 |
| Wanamaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Reli | 0 | 0 | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 |
| TAZARA | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Viwanja vya Ndege | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Bandari | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Tanzania Bara** | **74** | **2** | **15** | **1** | **4** | **0** | **1** | **344** | **441** |
| Kaskazini Pemba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini Unguja | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Kusini Pemba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini Unguja | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini Magharibi | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 8 | 12 |
| **Tanzania Zanzibar** | **3** | **0** | **1** | **0** | **0** | **4** | **0** | **8** | 16 |
| **Tanzania** | **77** | **2** | **16** | **1** | **4** | **4** | **1** | **352** | **457** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

### 2.3.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii

Jedwali Na. 3.9 linaonesha idadi na asilimia za ajali kulingana na vyanzo mbalimbali vya ajali katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025. Kati ya ajali hizo, ajali 614, zilitokana na sababu za kibinadamu sawa na asilimia 95.6, ajali 17 sawa na asilimia 2.6 zilisababishwa na ubovu wa vyombo vya usafiri, na sababu za kimazingira zilichangia ajali 11 sawa na asilimia 1.7.

**Jedwali Na. 3.9 Idadi ya Ajali kwa Vyanzo Vyake, Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Vyanzo vya Ajali kwa Makundi | Januari-Juni 2024 | | Januari-Juni 2025 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| **Sababu za Kibinadamu** | | | | |
| Uendeshaji wa hatari | 96 | 10.8 | 76 | 11.8 |
| Uzembe wa dereva | 359 | 40.5 | 288 | 44.9 |
| Uzembe wa M/baiskeli | 28 | 3.2 | 15 | 2.3 |
| Uzembe wa W/Pikipiki | 121 | 13.7 | 92 | 14.3 |
| Uzembe wa abiria | 0 | 0 | 2 | 0.3 |
| Mwendo kasi | 178 | 20.1 | 97 | 15.1 |
| Mifugo isiyochungwa | 0 | 0 | 1 | 0.2 |
| Kupita gari bila uangalifu | 40 | 4.5 | 19 | 3 |
| Uzembe wa W/miguu | 19 | 2.1 | 18 | 2.8 |
| Uzembe wa W/mikokoteni | 1 | 0.1 | 0 | 0 |
| Ulevi | 12 | 1.4 | 6 | 0.9 |
| **Jumla** | **854** | **96.4** | **614** | **95.6** |
| **Ubovu wa Vyombo vya Moto** | | | | |
| Ubovu wa gari | 25 | 2.8 | 17 | 2.6 |
| Hitilafu za Taa za magari barabarani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **25** | **2.8** | **17** | **2.6** |
| **Sababu za Mazingira** | | | | |
| Moto | 2 | 0.2 | 1 | 0.2 |
| Vizuizi vya njia | 1 | 0.1 | 1 | 0.2 |
| Ubovu wa barabara | 4 | 0.5 | 8 | 1.2 |
| Vivuko vya reli | 0 | 0 | 1 | 0.2 |
| **Jumla** | **7** | **0.8** | **11** | **1.7** |
| **Jumla Kuu** | **886** | **100** | **642** | **100** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

**Mchoro Na. 3.5 Vyanzo vya Ajali za Barabarani, Tanzania, Januari – Juni, 2025**



# SURA YA NNE

# UHUSIANO KATI YA UHALIFU NA VIGEZO VYA KIJAMII NA KIUCHUMI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia uhusiano uliopo baina ya makosa mbalimbali na vigezo vya kijamii, kiuchumi na utandawazi ambavyo vimekuwa vikichangia kuongezeka kwa idadi ya uhalifu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025. Baadhi ya vigezo hivyo ni kama vile idadi ya watu, ukubwa wa eneo na idadi ya askari. Tafiti mbalimbali zilizofanyika zinaonesha kuwa, kuna uhusiano mkubwa kati ya uhalifu na hali ya maisha ya watu pamoja na mazingira. Matokeo ya tafiti hizo yameliwezesha Jeshi la Polisi kubaini mbinu mbalimbali za kiuhalifu pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kudhibiti na kutanzua uhalifu na wahalifu nchini.

## 4.1 Uhusiano wa Uhalifu na Masuala ya Kijamii na Kiuchumi

Upo uhusiano wa karibu kati ya makosa yanayotendeka na idadi ya watu nchini, uhusiano huo kwa kawaida ni chanya, hii ikiwa na maana kuwa, mikoa yenye idadi kubwa ya watu ina idadi kubwa ya makosa tofauti na mikoa yenye watu wachache. Kutokana na makadirio ya idadi ya watu kwa mwaka 2024, Tanzania ina watu 66,278,276 na idadi ya makosa ya jinai yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 yalikuwa 293,890.

Kwa Tanzania Bara, ifuatayo ni baadhi ya mikoa inayoonesha uhusiano uliopo kati ya idadi ya watu na makosa yaliyoripotiwa; Dar es Salaam (Watu 5,739,734, Makosa 68,954), Mwanza (Watu 3,992,565, Makosa 26,206), Morogoro (Watu 3,405,761, Makosa 15,186), Kilimanjaro (Watu 1,976,588, Makosa 13,828), Mara (Watu 2,565,172, Makosa 13,664).

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, ifuatayo ni baadhi ya mikoa inayoonesha uhusiano uliopo kati ya idadi ya watu na makosa yaliyoripotiwa; Mjini Magharibi (Watu 962,135, Makosa 6,800) na Kusini Unguja (Watu 209,534, Makosa 1,563), (Jedwali Na. 6.1).

Vile vile upo uhusiano kati ya umaskini, idadi ya watu na kutendeka kwa uhalifu. Idadi ya watu au umaskini unapoongezeka, husababisha kuongezeka kwa uhalifu, na hii inatokana na kukosekana kwa kipato na kusababisha kuwepo kwa ongezeko la matukio ya uhalifu kwani watu hutumia njia zisizo halali ili kujipatia kipato.

## 4.2 Uhusiano wa Makosa ya Jinai, Idadi ya Watu na Eneo la Ardhi

### 4.2.1 Idadi ya makosa kwa Ukubwa wa Eneo.

Jedwali Na. 6.1 linaonesha kuwa Tanzania ina wastani wa Makosa Makubwa na Madogo 33 kwa kila kilomita 100 za mraba ambapo kwa Tanzania Bara ni wastani wa makosa 32 kwa kila kilomita 100 za mraba na kwa Tanzania Zanzibar ni wastani wa makosa 439 kwa kila kilomita 100 za mraba.

Hii inamaana kuwa, kuna baadhi ya maeneo askari wana majukumu makubwa ya kupambana na uhalifu. Hata hivyo uwiano huo wa makosa kwa eneo hutofautiana kati ya mkoa na mkoa.

Mikoa inayoongoza kuwa na uwiano mkubwa wa makosa kwa eneo la kilomita 100 za mraba kwa Tanzania Bara ni Dar es Salaam (6,895), Mwanza (291), Kilimanjaro (106), Mara (62) na Geita (50). Tanzania Zanzibar mikoa inayoongoza kuwa na Uwiano Mkubwa wa Makosa kwa eneo la kilomita 100 za mraba ni Mjini Magharibi (2,957), Kusini Pemba (237) na Kaskazini Unguja (236).

Mikoa yenye uwiano mkubwa wa makosa makubwa kwa eneo la kilomita 100 za mraba kwa Tanzania Bara ni Dar es Salaam (366), Mwanza (12), Kilimanjaro, Mara (9 kila mmoja) na Pwani (5). Mikoa yenye uwiano mkubwa wa makosa makubwa kwa eneo la kilomita 100 za mraba kwa Tanzania Zanzibar ni Mjini Magharibi (226), Kusini Pemba (43) na Kaskazini Unguja (34). Idadi kubwa ya uwiano wa makosa kwa kila kilomita 100 inachangiwa na baadhi ya maeneo kuwa na shughuli nyingi za kiuchumi.

### 4.2.2 Uwiano wa Makosa kwa kila Watu 100,000

Idadi ya watu katika eneo moja huchangia ongezeko au upungufu wa makosa. Iwapo idadi ya watu inaongezeka inatakiwa iendane na ongezeko la askari Polisi. Kuongezeka kwa idadi ya askari itasaidia kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu. Idadi ya askari inapokuwa kubwa inasaidia kuwepo kwa amani na utulivu ambao unawezesha watu kutumia muda wao vizuri katika shughuli za uzalishaji mali na ufanyaji wa biashara ili kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Mikoa inayoongoza kuwa na makosa makubwa na madogo kwa kila watu 100,000 Tanzania Bara ni Dar es Salaam (makosa 1,201), Kilimanjaro (makosa 700), Mwanza (makosa 656), Pwani (makosa 546) na Mara (makosa 533), na mikoa yenye idadi ndogo ya makosa kwa kila watu 100,000 Tanzania Bara ni Simiyu (makosa 123), Kigoma (makosa 220), Rukwa (225), Kagera (makosa 236) na Lindi (240). Mikoa inayoongoza kuwa na makosa makubwa na madogo kwa kila watu 100,000 Tanzania Zanzibar ni Kusini Unguja (makosa 746) na Mjini Magharibi (makosa 707), na mikoa yenye idadi ndogo ya makosa kwa kila watu 100,000 Tanzania Zanzibar ni Kaskazini Pemba (Makosa 180) na Kusini Pemba (268), (Jedwali Na. 4.1).

**Jedwali Na. 4.1 Idadi ya Makosa, Idadi ya Watu kwa kila Kosa, Makosa ya Jinai kwa kila Kilomita 100 za Mraba na Uwiano wa Makosa kwa Kila Watu 100,000 kwa Mkoa; Tanzania, Januari - Juni, 2025**

| Mkoa | Makosa Makubwa Jinai | Makosa Madogo Jinai | Makosa Yote Jinai | Idadi ya Watu | Makosa Makubwa / Watu 100,000 | Jinai Yote / $Km^2$ 100 | Jinai Yote / Watu 100,000 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 1,034 | 11,615 | 12,649 | 2,524,141 | 41 | 33 | 501 |
| Dar es Salaam | 3,658 | 65,296 | 68,954 | 5,739,734 | 64 | 6,895 | 1,201 |
| Dodoma | 1,024 | 9,774 | 10,798 | 3,300,186 | 31 | 26 | 327 |
| Geita | 181 | 9,874 | 10,055 | 3,241,053 | 6 | 50 | 310 |
| Iringa | 428 | 4,770 | 5,198 | 1,260,104 | 34 | 15 | 413 |
| Kagera | 955 | 6,649 | 7,604 | 3,226,032 | 30 | 30 | 236 |
| Katavi | 270 | 3,600 | 3,870 | 1,253,158 | 22 | 9 | 309 |
| Kigoma | 607 | 5,272 | 5,879 | 2,669,703 | 23 | 16 | 220 |
| Kilimanjaro | 1,222 | 12,606 | 13,828 | 1,976,588 | 62 | 106 | 700 |
| Lindi | 295 | 2,733 | 3,028 | 1,262,641 | 23 | 5 | 240 |
| Manyara | 627 | 7,858 | 8,485 | 2,035,641 | 31 | 19 | 417 |
| Mara | 1,992 | 11,672 | 13,664 | 2,565,172 | 78 | 62 | 533 |
| Mbeya | 840 | 9,591 | 10,431 | 2,495,901 | 34 | 28 | 418 |
| Morogoro | 1,043 | 14,143 | 15,186 | 3,405,761 | 31 | 21 | 446 |
| Mtwara | 429 | 4,004 | 4,433 | 1,738,231 | 25 | 26 | 255 |
| Mwanza | 1,043 | 25,163 | 26,206 | 3,992,565 | 26 | 291 | 656 |
| Pwani | 1,789 | 9,931 | 11,720 | 2,144,928 | 83 | 36 | 546 |
| Njombe | 317 | 2,598 | 2,915 | 939,503 | 34 | 14 | 310 |
| Rukwa | 446 | 3,339 | 3,785 | 1,680,335 | 27 | 16 | 225 |
| Ruvuma | 442 | 4,387 | 4,829 | 1,982,240 | 22 | 8 | 244 |
| Shinyanga | 262 | 7,195 | 7,457 | 2,410,306 | 11 | 39 | 309 |
| Simiyu | 232 | 2,643 | 2,875 | 2,338,396 | 10 | 12 | 123 |
| Singida | 287 | 5,341 | 5,628 | 2,166,130 | 13 | 11 | 260 |
| Songwe | 393 | 3,865 | 4,258 | 1,444,855 | 27 | 19 | 295 |
| Tabora | 733 | 8,650 | 9,383 | 3,657,677 | 20 | 12 | 257 |
| Tanga | 1,094 | 8,536 | 9,630 | 2,790,841 | 39 | 36 | 345 |
| **Tanzania Bara** | **21,643** | **261,105** | **282,748** | **64,241,822** | **34** | **32** | **440** |
| Kaskazini Unguja | 160 | 951 | 1,111 | 275,531 | 58 | 236 | 403 |
| Kusini Unguja | 265 | 1,298 | 1,563 | 209,534 | 126 | 183 | 746 |
| Mjini Magharibi | 519 | 6,281 | 6,800 | 962,135 | 54 | 2,957 | 707 |
| Kaskazini Pemba | 121 | 411 | 532 | 295,724 | 41 | 93 | 180 |
| Kusini Pemba | 143 | 644 | 787 | 293,530 | 49 | 237 | 268 |
| **Tanzania Zanzibar** | **1,208** | **9,585** | **10,793** | **2,036,454** | **59** | **3,706** | **530** |
| Vikosi Vingine | 69 | 280 | 349 | | | | |
| **Tanzania** | **22,920** | **270,970** | **293,890** | **66,278,276** | **35** | **33** | **443** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

## 4.3 Matukio ya Usalama Barabarani

Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, jumla ya matukio makubwa na madogo ya usalama barabarani 1,359,468 yaliripotiwa. Matukio makubwa yalikuwa 642 (asilimia 0.05) ya makosa yote na makosa madogo yalikuwa 1,358,826 (asilimia 99.95). Jeshi la Polisi lina idadi ya askari 4,333 wa kikosi cha usalama barabarani ikilinganishwa na idadi ya askari 4,119 kwa kipindi kama hicho 2024, sawa na ongezeko la askari 214. Hii ina maana kuwa askari mmoja alishughulikia makosa 314 ya usalama barabarani kwa kipindi hicho 2025.

Jedwali Na. 4.2 linaonesha uwiano wa makosa ya usalama barabarani kwa askari wa kikosi hicho. Uwiano huu unatofautiana baina ya mkoa na mkoa, ambapo mikoa yenye uwiano mkubwa Tanzania Bara ni Dar es Salaam (1:554), Arusha (1:461), Mwanza (1:455), Geita (1:453) na Manyara (1:426). Mikoa yenye uwiano mdogo ni Songwe (1:127), Tanga (1:154), Dodoma (1:163), Simiyu (1:166) na Ruvuma (1:201). Mikoa yenye uwiano mkubwa Tanzania Zanzibar ni Kaskazini Unguja (1:138) na Mjini Magharibi (1:107). Mikoa yenye uwiano mdogo ni Kaskazini Pemba (1:31) na Kusini Pemba (1:44).

Mikoa inayoongoza kuwa na uwiano mkubwa wa makosa kwa eneo la kilomita 100 za mraba Tanzania Bara ni Dar es Salaam (32,881), Mwanza (733), Pwani (419), Kilimanjaro (253) na Geita (231). Mikoa yenye idadi ndogo ya makosa ni Ruvuma (32), Katavi (34), Lindi (38), Singida (57) na Songwe (62). Mikoa yenye idadi kubwa ya makosa kwa eneo la kilomita 100 za mraba Tanzania Zanzibar ni Mjini Magharibi (6,403) na Kaskazini Unguja (1,351) na mikoa yenye idadi ndogo ni Kaskazini Pemba (186) na Kusini Pemba (385).

**Jedwali Na. 4.2 Idadi ya Matukio ya Usalama Barabarani, Idadi ya Watu na Askari, Uwiano wa Makosa kwa kila kilometa 100 za Mraba na Matukio kwa kila Askari kwa Mkoa; Tanzania, Januari - Juni, 2025**

| Mkoa | Matukio ya usalama barabarani | Idadi ya watu | Idadi ya askari | Makosa/$km^2_{100}$ | Matukio/Askari |
|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 59,444 | 2,524,141 | 129 | 156 | 461 |
| Dar es Salaam | 328,935 | 5,739,734 | 593 | 32,881 | 554 |
| Dodoma | 36,037 | 3,300,186 | 221 | 88 | 163 |
| Geita | 46,244 | 3,241,053 | 102 | 231 | 453 |
| Iringa | 49,711 | 1,260,104 | 141 | 142 | 352 |
| Kagera | 32,159 | 3,226,032 | 136 | 129 | 236 |
| Katavi | 15,112 | 1,253,158 | 65 | 34 | 232 |
| Kigoma | 33,712 | 2,669,703 | 150 | 91 | 225 |
| Kilimanjaro | 32,885 | 1,976,588 | 142 | 253 | 231 |
| Lindi | 25,272 | 1,262,641 | 90 | 38 | 281 |
| Manyara | 53,231 | 2,035,641 | 125 | 118 | 426 |
| Mara | 38,220 | 2,565,172 | 149 | 174 | 256 |
| Mbeya | 58,730 | 2,495,901 | 173 | 159 | 339 |
| Morogoro | 89,152 | 3,405,761 | 264 | 126 | 338 |
| Mtwara | 22,661 | 1,738,231 | 101 | 133 | 224 |
| Mwanza | 65,949 | 3,992,565 | 145 | 733 | 455 |
| Njombe | 32,017 | 2,144,928 | 100 | 97 | 320 |
| Pwani | 87,931 | 939,503 | 249 | 419 | 353 |
| Rukwa | 35,172 | 1,680,335 | 104 | 153 | 338 |
| Ruvuma | 20,754 | 1,982,240 | 103 | 32 | 201 |
| Shinyanga | 31,856 | 2,410,306 | 97 | 168 | 328 |
| Simiyu | 16,291 | 2,338,396 | 98 | 65 | 166 |
| Singida | 28,152 | 2,166,130 | 128 | 57 | 220 |
| Songwe | 14,382 | 1,444,855 | 113 | 62 | 127 |
| Tabora | 51,020 | 3,657,677 | 146 | 67 | 349 |
| Tanga | 25,503 | 2,790,841 | 166 | 94 | 154 |
| **Tanzania Bara** | **1,330,542** | **64,241,822** | **4,030** | **151** | **330** |
| Kaskazini Unguja | 6,383 | 275,531 | 46 | 1,351 | 138 |
| Kusini Unguja | 5,417 | 209,534 | 57 | 632 | 95 |
| Mjini Magharibi | 14,759 | 962,135 | 137 | 6,403 | 107 |
| Kaskazini Pemba | 1,074 | 295,724 | 34 | 186 | 31 |
| Kusini Pemba | 1,293 | 293,530 | 29 | 385 | 44 |
| **Tanzania Zanzibar** | **28,926** | **2,036,454** | **303** | **1,172** | **95** |
| **Tanzania** | **1,359,468** | **66,278,276** | **4,333** | **154** | **314** |

*Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania*

# SURA YA TANO

# MIKAKATI YA KUKABILIANA NA UHALIFU NA MATUKIO YA USALAMA BARABARANI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inaonesha aina ya makosa, vyanzo na mikakati ya kukabiliana na hali ya uhalifu katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025. Takwimu ni muhimu katika kuandaa mipango ya kubaini, kuzuia, kudhibiti, kutanzua, kuainisha na kuanzisha mikakati mipya, kuboresha mikakati iliyopo pamoja na kupata rasilimali watu, fedha na vifaa vya kutosha kutoka Serikalini na kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutokomeza uhalifu na kupunguza ajali za barabarani nchini.

Sura hii inatumia takwimu zilizochambuliwa katika sura zilizotangulia kuelezea mikakati ya kukabiliana na makosa yafuatayo: -

i. Makosa dhidi ya binadamu,
ii. Makosa ya kuwania mali,
iii. Makosa dhidi ya maadili ya jamii,
iv. Makosa ya uhalifu wa kifedha,
v. Matukio ya usalama barabarani,
vi. Makosa kwa njia ya mtandao.

Mikakati ya kudhibiti na kupambana na makosa ya Jinai na matukio ya Usalama Barabarani imeainishwa kwenye Jedwali Na. 5.1, 5.2, 5.3, 5.4, 5.5 na 5.6.

## 5.1 Makosa Dhidi ya Binadamu

**Jedwali Na. 5.1 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari - Juni, 2025**

| Makosa Dhidi ya Binadamu | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari - Juni, 2025 )** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Mauaji | 926 | i. Wivu wa mapenzi/ugoni<br>ii. Visasi<br>iii. Tamaa ya kupata mali kinyume cha sheria<br>iv. Ulevi<br>v. Migogoro ya ardhi/mali<br>vi. Imani za kishirikina<br>i. Kujichukulia sheria mkononi | i. Kuelimisha jamii kuachana na vitendo vya kishirikina vya mauaji ya watoto, wazee na albino.<br>ii. Kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali ili jamii ibadilike na kuacha kujichukulia sheria mkononi.<br>iii. Kuhamasisha jamii ili ijihusishe na shughuli zilizo halali katika kujipatia kipato.<br>iv. Jeshi la Polisi kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro katika jamii.<br>v. Kushirikisha Taasisi za kidini, wazee wakimila/machifu na wadau mbalimbali katika kuhamasisha jamii ili kuachana na imani potofu za kishirikina.<br>vi. Kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwa madhumuni ya kuimarisha utoaji wa elimu rika kwa vijana ili waweze kuzikabili changamoto za mahusiano ya kijinsia.<br>vii. kuhamasisha jamii kuwatumia watalaamu wa Ushauri nasihi pindi wanapopatwa na changamoto za afya ya akili na migogoro mbalimbali katika jamii. |

**Makosa Dhidi ya Binadamu**

| Aina ya Kosa | Idadi ya Makosa (Januari - Juni, 2025 ) | Chanzo | Mikakati |
|---|---|---|---|
| 2. Kubaka | 3,938 | i. Tamaa za kimwili<br>ii. Mmomonyoko wa maadili<br>iii. Imani za kishirikina.<br>iv. Utandawazi<br>v. Ulevi<br>vi. Kisasi | i. Kuendelea kuielimisha jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa sheria mbalimbali hususani Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Mwaka 2015.<br>ii. Kuelimisha jamii kuzingatia na kufuata maadili ya Kitanzania.<br>iii. Kushirikisha Taasisi za kidini, wazee wakimila/machifu na wadau mbalimbali katika kuhamasisha jamii ili kuachana na imani potofu za kishirikina.<br>iv. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, kutenga muda maalumu mashuleni/vyuoni kutoa elimu ya ulinzi wa fikra kwa watoto ili waweze kutambua viashiria vya watu wenye nia mbaya mfano kampeni ya *''TUWAAMBIE KABLA HAWAJAHARIBIWA''*.<br>v. Kuendelea kukusanya taarifa za kiintelijensia ili kubaini mtu/watu au kikundi/taasisi zinazochochea na kufadhili wahalifu wa makosa haya na upotoshaji wa maadili ya kitanzania na kuchukua hatua za kisheria. |
| 3. Kulawiti | 997 | | |
| 4. Kutupa Watoto | 80 | i. Matatizo ya kiuchumi<br>ii. Tatizo la afya ya akili<br>iii. Hofu ya kutengwa na familia<br>iv. Kutelekezwa<br>v. Imani potofu | i. Kushirikiana na taasisi za kidini ili kutoa elimu ya kiroho (spiritual patrol) ili watu wawe na hofu ya Mungu na kuachana na imani potofu.<br>ii. Kutoa elimu kwa jamii kupitia wadau mbalimbali ili jamii ipate uelewa wa kutokuwatenga na kuwatelekeza watoto.<br>iii. Kutoa elimu kupitia Polisi Jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili jamii ijiepushe na mimba za utotoni/.<br>iv. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Afya zitoe elimu ya afya ya akili kwa makundi mbalimbali katika jamii. |
| 5. Wizi wa Watoto | 44 | i. Ugumba.<br>ii. Imani ya kishirikina<br>iii. Kipato | i. Kushirikisha Taasisi za kidini, wazee wakimila/machifu na wadau mbalimbali katika kuhamasisha jamii ili kuachana na imani potofu za kishirikina.<br>ii. Kushirikisha Wizara ya Afya kutoa elimu ya uzazi na ustawi wa jamii kwa wananchi.<br>iii. Kuhamasisha jamii ili ijihusishe na shughuli zilizo halali katika kujipatia kipato. |
| 6. Usafirishaji Haramu wa Binadamu | 3 | i. Tamaa ya kujipatia kipato<br>ii. Umasikini<br>iii. Utandawazi<br>iv. Ukosefu wa elimu<br>v. Ukosefu wa taarifa sahihi | i. Kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia ofisi za ubalozi, Idara ya uhamiaji pamoja na wadau wengine kama taasisi za kimataifa mfano IOM na INTERPOL katika kudhibiti biashara haramu ya kusafirisha binadamu.<br>ii. Kutoa elimu kwa jamii kupitia NGO's mbalimbali juu ya athari za biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.<br>iii. Kuelimisha jamii juu ya usahihi wa taarifa zilizopo mitandaoni kuhusiana na fursa zinazotangazwa mfano ajira, ufadhili wa masomo nk. |

## 5.2 Makosa ya Kuwania Mali

**Jedwali Na. 5.2 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa ya Kuwania Mali kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni, 2025**

| Makosa ya Kuwania Mali | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari - Juni, 2025 )** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Unyang'anyi wa Kutumia Silaha | 127 | i. Hali duni ya kiuchumi.<br>ii. Ukuaji wa miji.<br>iii. Utandawazi.<br>iv. Tofauti kubwa ya hali ya maisha kati ya walionacho na wasionacho.<br>v. Uhaba wa ajira kwa vijana.<br>vi. Tamaa ya kumiliki mali. | i. Kuhamasisha jamii hususani vijana kushiriki katika shughuli halali za ujasiriamali/uchumi ili kujipatia kipato.<br>ii. Kuzishawishi taasisi za fedha ili ziweze kupunguza urasimu wa upatikanaji wa mikopo nafuu na kupunguza riba kubwa zinazotozwa katika mikopo hiyo.<br>iii. Kuwepo na mipango endelevu ya utoaji elimu kwa umma hususani elimu ya ujasiriamali.<br>iv. Kuhamasisha jamii ijenge utamaduni na utaratibu wa kutoa taarifa kwa wakati kwenye vyombo vya dola wanapobaini viashiria vya uhalifu na wahalifu.<br>v. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuibua fursa kwa vijana ili kujipatia kipato na kuepukana na vishawishi vya kujiingiza kwenye uhalifu.<br>vi. Jeshi la Polisi kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuelimisha jamii ya wafugaji juu ya umuhimu wa uwekaji alama za utambuzi wa mifugo yao.<br>vii. Kuendelea kupiga marufuku machinjio na minada isiyo rasmi. |
| 2. Unyang'anyi wa Kutumia Nguvu | 278 | | |
| 3. Uvunjaji | 4,227 | | |
| 4. Wizi | 236 | | |
| 5. Wizi wa Pikipiki | 2,003 | | |
| 6. Wizi wa Magari | 29 | | |
| 7. Wizi wa Mifugo | 1,749 | | |
| 8. Kuchoma Nyumba Moto | 255 | i. Visasi<br>ii. Hujuma<br>iii. Tamaa ya kupata fidia ya uharibifu wa mali (bima). | i. Kuimarisha matumizi ya Intelijensia ili kubaini viashiria vya migogoro kabla ya madhara kutokea.<br>ii. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa jamii kutumia njia sahihi za kupata haki zao.<br>iii. Kuendelea kutoa ushauri kwa Mashirika ya bima juu ya kufanya uchunguzi wa kutosha kabla ya kuidhinisha fidia |

## 5.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii

**Jedwali Na. 5.3 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti, Kutanzua Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Juni, 2025**

<table>
<tr><th colspan="4">Makosa Dhidi ya Maadili</th></tr>
<tr><th>Aina ya Kosa</th><th>Idadi ya Makosa (Januari -Juni 2025)</th><th>Chanzo</th><th>Mikakati</th></tr>
<tr><td>1. Kupatikana na Silaha</td><td>104</td><td>i. Hali duni ya kiuchumi.<br>ii. Ujangili.<br>iii. Umiliki holela wa silaha za viwandani na kienyeji.<br>iv. Migogoro ya kisiasa/kivita katika baadhi ya nchi za jirani.<br>Uzagaaji wa silaha zinazotokana na viashiria vya ugaidi.</td><td>i. Kuendelea kushirikiana na jamii kutumia falsafa ya Polisi Jamii katika mapambano dhidi ya uhalifu na wahalifu.<br>ii. Kushirikiana na wadau mbalimbali kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mipaka ili kubaini wageni wanaoingia na kutoka nchini.<br>iii. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umiliki halali wa silaha.<br>iv. Kuendelea kuhimiza usalimishaji wa hiari wa silaha zisizomilikiwa kihalali.<br>v. Uwekaji wa alama za utambuzi kwenye Silaha na kuendelea kuimarisha kanzi data ya silaha zote<br>vi. Kuendelea kutekeleza mikataba na itifaki za kimataifa juu ya kudhibiti uzagaaji holela wa silaha ndogo na nyepesi.<br>vii. Kuendelea kukusanya taarifa za kiintelijensia/fiche juu ya umiliki wa silaha kinyume cha sheria</td></tr>
<tr><td>2. Kupatikana na Dawa za kulevya za viwandani</td><td>14</td><td rowspan="5">i. Tamaa ya kipato na mali.<br>ii. Kukosa maadili<br>iii. Sababu za kimazingira na makundi mabaya.<br>iv. Uhaba wa ajira<br>v. Uwepo wa bandari bubu na njia haramu maeneo ya mipakani.<br>i. Ukinzani wa sheria baina ya nchi za ukanda mmoja.</td><td rowspan="5">i. Kushirikiana na nchi jirani kufanya operesheni na misako dhidi ya uhalifu unaovuka mipaka.<br>ii. Kushirikisha wadau mbalimbali kuelimisha jamii juu ya athari za dawa za kulevya.<br>iii. Kuwahamasisha vijana kushiriki katika shughuli halali za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni<br>iv. Kuendeleza operesheni na misako ya mara kwa mara kwenye maeneo tete.<br>v. Kushirikisha wazazi na walezi katika ngazi ya familia, shule na vyuo kwa kutoa elimu na mafunzo ya maadili na ya uraia.<br>vi. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira ili kutunza na kuhifadhi rasilimali za nchi yetu.<br>vii. Kuendelea kuwapatia mafunzo askari wanaopita katika vyuo vya Polisi, juu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya.<br>viii. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa/Shehia kuwatambua na kuwadhibiti watengenezaji, wauzaji, na wasambazaji wa pombe ya moshi.</td></tr>
<tr><td>3. Kupatikana na Bhangi</td><td>2,881</td></tr>
<tr><td>4. Kupatikana na Mirungi</td><td>657</td></tr>
<tr><td>5. Kupatikana na Nyara za Serikali</td><td>353</td></tr>
<tr><td>6. Kupatikana na Pombe ya Moshi</td><td>2,433</td></tr>
<tr><td>7. Wahamiaji Haramu</td><td>418</td><td>i. Tamaa ya kipato na mali.<br>ii. Migogoro ya kisiasa katika nchi jirani.</td><td>i. Kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mipaka ili kubaini wahamiaji haramu.<br>ii. Kuendeleza ushirikiano na Majeshi ya Polisi kupitia jumuiya za kikanda na kimataifa (EAPCCO, SARPCCO, AFRIPOL na INTERPOL)<br>iii. kukabiliana na uhalifu unaovuka mipaka.</td></tr>
</table>

## 5.4 Makosa ya Kifedha

**Jedwali Na. 5.4: Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti, Kutanzua Makosa ya Kifedha kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari - Juni, 2025**

| Makosa ya Kifedha | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari - Juni, 2025)** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Kupatikana na Noti Bandia | 77 | i. Hali duni ya kiuchumi.<br>ii. Mmomonyoko wa maadili.<br>iii. Utandawazi na Ukuaji wa teknolojia.<br>iv. Ukuaji wa miji.<br>v. Uhaba wa ajira.<br>vi. Tamaa ya kujipatia kipato na mali.<br>vii. Umasikini | i. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuzuia makosa ya kifedha kama vile utakatishaji fedha na makosa ya kimtandao.<br>ii. Kuhamasisha umma na wadau mbalimbali katika kuwatia moyo vijana kujihusisha na shughuli halali za kiuchumi na kijamii.<br>iii. Kuzishawishi Taasisi za fedha kupunguza urasimu wa upatikanaji wa mikopo na kupunguza riba kubwa zinazotozwa kwenye mikopo hiyo.<br>iv. Kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kujiajiri hasa kwa vijana.<br>v. Jeshi la Polisi kutoa elimu au ushauri katika vyama vya ushirika ambavyo sio vya kiserikali kuajiri watu wenye taaluma katika taasisi za fedha.<br>vi. Wapelelezi wapewe mafunzo ya kisasa yanayohusiana na makosa ya kifedha. |
| 2. Kughushi | 352 | | |
| 3. Wizi katika Serikali Kuu | 4 | | |
| 4. Wizi katika Serikali za Mitaa | 4 | | |
| 5. Wizi katika Mashirika ya Umma. | 16 | | |

## 5.5 Makosa ya Kimtandao

**Jedwali Na. 5.5 Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa ya Kimtandao kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni 2025**

| Makosa ya Kimtandao | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari -Juni, 2025 )** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Makosa ya kimtandao (Kuingilia mfumo kinyume cha sheria, Kubakia kwenye mfumo kinyume cha sheria, Ujasusi wa data, Picha za ngono na Kula njama kwa nia ya kutenda kosa) | 497 | i. Hali duni ya kiuchumi.<br>ii. Kukosa maadili.<br>iii. Utandawazi na ukuaji wa teknolojia.<br>iv. Uhaba wa ajira kwa vijana.<br>v. Tamaa ya kujipatia kipato/ mali. | i. Kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kuzuia makosa ya kimtandao.<br>ii. Kuelimisha watumiaji wa mitandao juu ya usiri na umuhimu wa kutomwamini mtu kuhusu nywila (neno la siri) zao.<br>iii. Kuendelea kutoa elimu ya sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka, 2020 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023.<br>iv. Jeshi la Polisi kutumia vifaa vya kisasa vya kufatilia miamala ya kidijitali, mitandao ya kijamii na mifumo ya TEHAMA ili kubaini na kutanzua makosa ya kimtandao kabla hayajatokea.<br>v. Kuangalia upya mitaala iliyopo katika vyuo vya Polisi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na uhalifu wa kisasa (upelelezi wa kidijitali, usalama wa mitandao na uchambuzi wa ushahidi wa kieletroniki. |
| 2. Wizi (Kuhamisha fedha kwa mtandao, simbanking, ATM, kuamisha fedha kwa kutumia simu) | 1,559 | | |

## 5.6 Matukio ya Ajali za Barabarani

**Jedwali Na. 5.6: Idadi ya Makosa na Mikakati Inayotumika Kubaini, Kuzuia, Kudhibiti na Kutanzua Makosa ya Ajali za Barabarani kwa Aina ya Kosa; Tanzania, Januari – Juni 2025**

| Matukio ya Ajali za Barabarani | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari -Juni, 2025)** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Ajali za barabarani | 642 | i. Ukosefu wa elimu ya usalama barabarani kwa baadhi ya watumiaji wa vyombo vya moto.<br>ii. Kutofuata Sheria za usalama barabarani.<br>iii. Uchakavu wa vyombo vya usafiri.<br>iv. Ubovu wa miundombinu ya barabara.<br>v. Ulevi.<br>vi. Uzembe.<br>vii. Uwepo wa vipuri visivyokidhi viwango.<br>viii. Mwendokasi | i. Kuendelea kudhibiti mwendokasi kwa kutumia mifumo mbalimbali iliyopo ndani ya Jeshi la Polisi. Mfano; VTS.<br>ii. Kuimarisha doria na ukaguzi barabarani.<br>iii. Kuendelea kutoa adhabu stahiki kwa wakosaji kwa mujibu wa Sheria ya usalama barabarani Sura ya 168.<br>iv. Kuendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kwa watumiaji mbalimbali wa barabara.<br>v. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kuwa wamiliki wa vyombo vya usafiri wana ajiri watu wenye ujuzi, weledi na maadili ili kupunguza ajali zinazoepukika.<br>vi. Ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri.<br>vi. Kuwajengea uwezo askari wa usalama barabarani ili wafanye kazi kwa maadili na weledi kwa kuwapatia vifaa vya kisasa.<br>vii. Kuzishauri mamlaka zinazosimamia miundombinu ya barabara kufanya matengenezo na marekebisho ya mara kwa mara. |
| Ajali zilizosababisha vifo | 443 | | |
| Ajali zilizosababisha majeruhi | 176 | | |
| Ajali za kawaida | 23 | | |
| 2. Watu waliokufa | 640 | | |
| 3. Watu waliojeruhiwa | 1,100 | | |

# SURA YA SITA

# MATUKIO YALIYOVUTA HISIA KWA JAMII.

## 6.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea matukio ya uhalifu na usalama barabarani yaliyovuta hisia katika jamii. Matukio haya ni yale ambayo kutokea kwake husababisha mshtuko na kuvuta hisia kwa jamii.
Yafuatayo ni matukio yakushtua ambayo yalivuta hisia kwa jamii katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 kama yalivyoripotiwa kutoka sehemu mbalimbali nchini.

**1. Manyara**

**Baba wa kambo amuua mtoto baada ya mtoto kumlilia mama yake.**

Mnamo 10/01/2025 Majira ya saa kumi na mbili jioni huko katika Kitongoji cha Sandege Kijiji cha Loltepesi, Kata na Tarafa ya Sunya Wilaya ya kiteto na Mkoa wa Manyara. Mtoto wa Miaka 5, mkazi wa kijiji cha Loltepesi aliuawa kwa kupigwa na kitu butu sehemu mbalimbali za mwili wake na kuvunjwa shingo na baba yake wa kambo/mlezi, Mrangi, miaka 23, mkulima mkazi wa Loltepesi. Chanzo cha tukio hilo ni baada ya mtoto huyo (marehemu) kumlilia mama yake mzazi wakati anakwenda hospitali. Mtuhumiwa amekamatwa na kufikishwa mahakamani.

**2. Tanga**

**Baba amuua binti yake kwa kumpiga na kitu butu kisha kumvunja shingo na kumning'iniza juu ya paa la nyumba.**

Mnamo 13/02/2025 majira ya saa moja kamili asubuhi huko Kitongoji cha Machenya, Kijiji cha Mkomba, Kata ya Kwachaga, Tarafa ya Magamba, Wilaya ya Handeni na Mkoa wa Tanga. Msichana mwenye miaka 16, mkulima na mkazi wa Machenye - Mkomba aliuawa na baba yake mzazi mwenye miaka 37, mkulima wa Machenye - Mkomba baada ya kumpiga na kitu butu sehemu mbalimbali za mwili wake hadi kumuua, alimvunja shingo na kuchukua kipande cha kanga kisha kumning'iniza juu ya paa la nyumba na kuwatangazia majirani zake kwamba mtoto wake amejinyonga kwa lengo la kukwepa mkono wa sheria. Chanzo cha tukio ni ugomvi kati ya marehemu na mama yake wa kambo. Mtuhumiwa amekamatwa na kufikishwa mahakamani.

**3. Iringa**

**Mume amuua mke wake Ukweni.**

Mnamo 11/03/2025 majira ya saa nane kamili usiku, huko katika Kitongoji cha Isimike kilichopo Kijiji na Kata ya Ukumbi, Tarafa na Wilaya ya Kilolo Mkoa wa Iringa, Mwanamke mwenye miaka 48, Mhehe, mkulima wa Njombe aliuawa kwa kuchomwa na kisu tumboni hadi utumbo kutoka nje na mume wake mwenye wa miaka 28, Mbena, mkulima wa Njombe ambaye yeye alijichoma na kisu hicho tumboni na kufariki. Awali, walikwenda nyumbani kwa mama wa mke wake kwa ajili ya kusuluhishwa mgogoro wao wa ndoa, ambapo usiku wakiwa nyumbani hapo ndipo muthumiwa alitenda tukio hilo. Kiini cha tukio ni mgogoro wa ndoa.

**4. Ruvuma**

**Mtoto wa kike wa miezi saba auliwa na baba yake.**

Mnamo 12/03/2025 majira ya saa mbili usiku huko Kitongoji cha Mpakani, Kijiji na Kata ya Muhongozi, Tarafa ya Kigonsera, Wilaya ya Mbinga na Mkoa wa Ruvuma. Mtoto mdogo wa kike mwenye umri wa miezi saba wa Kijiji cha Muhongozi aliuawa kwa kupigizwa kichwa chini na baba yake mzazi, Mkazi wa kijiji cha Muhongozi mbinu aliyoitumia ni kumnyang'anya mkewe mtoto, kumning'iniza kichwa chini miguu juu kisha kumpigiza ardhini kwa nguvu, Chanzo cha tukio hilo ni ugomvi wa kifamilia kati ya mume na mke. Mtuhumiwa amefikishwa mahakamani.

**5. Pwani**

**Akatwa uume wake na korodani moja na baba yake mdogo.**

Mnamo 01/04/2025 majira ya saa nane kamili mchana huko Ubena Wilaya ya Kipolisi Chalinze Mkoa wa Pwani, Mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 13, mwanafunzi wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Ubena, mkazi wa ubena alijeruhiwa kwa kukatwa uume na korodani moja la upande wa kushoto na kitu chenye ncha kali na baba yake mdogo na kisha kutoweka navyo. Awali, madhura aliongozana na baba yake mdogo kwenda porini kukata kuni ndipo wakiwa katika harakati za kuokota kuni ghafla baba yake mdogo alimvamia kwa nyuma na kumuwekea kitambaa puani kinachosadikika kuwa na dawa kilichomfanya apoteze fahamu na alipozinduka alijikuta yupo uchi huku akiwa na maumivu sehemu za siri kisha alivaa nguo zake na kurudi nyumbani ambapo hakumueleza mtu yeyote mpaka kesho yake jioni baba yake mkubwa aligundua tatizo hilo baada ya mhanga kushindwa kwenda shule na kumkuta anavuja damu sehemu za siri. Mtuhumiwa anatafutwa.

**6. Manyara**

**Mtoto amuua mama yake mzazi.**

Mnamo 12/04/2025 majira ya saa nne kamili asubuhi huko katika kitongoji cha Mji Mpya Kijiji cha Orongadida Kata ya Qashi Tarafa na wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara Mwanamke mwenye miaka 57, Mrangi, mkulima na Mkazi wa Kijiji cha Orongadida aliuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali shingoni na mtoto wake Mwanaume mwenye miaka 34, Msukuma, mkulima na mkazi wa Orongadida. Chanzo kuwania mali ya urithi ambapo mtuhumiwa alikuwa anataka mama yake aondoke kwenye nyumba ili aweze kurithi. Mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

**7. Kagera**

**Baba mzazi ambaka mtoto wake na kumlawiti.**

Mnamo tarehe 12/04/2025 majira ya saa moja na nusu usiku huko mtaa wa Ntungami kata ya Busimbe Tarafa ya Rwamishenye Manispaa ya Bukoba na Mkoa wa Kagera Mtoto wa kike mwenye wa umri miaka 12 Mwanafunzi wa darasa la sita Shule ya msingi Ihungo alibakwa na kulawitiwa na baba yake mzazi mwenye umri wa miaka 58, mkulima na mkazi wa mtaa wa Ntungamo. Chanzo cha tukio ni mmomonyoko wa maadili, mtuhumiwa amefikishwa mahakamani.

**8. Kilimanjaro**

**Mume amuua mke wake kwa kumchoma kisu mara kumi.**

Mnamo 18/04/2025 majira ya saa tatu asubuhi huko Marangu halisi kisawe, Kata ya Marangu Mashariki, Tarafa ya Vunjo Mashariki, Wilaya ya Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro. Mwanamke mwenye umri wa miaka 27, Mkazi wa Marangu Halisi, aliuawa kwa kuchomwa na kisu mgongoni na shingoni mara kumi na mume wake Mwenye umri wa miaka 32, mkulima, Mkazi wa Marangu Halisi. Chanzo cha tukio ni wivu wa mapenzi baada ya kumhisi mke wake kuwa ana mahusiano ya kimapenzi na mwanaume mwingine. Mtuhumiwa alijiua kwa kujichoma na kisu tumboni kwa lengo la kupoteza ushahidi.

**9. Manyara**

**Amuua baba yake na kumkata sehemu zake za siri.**

Mnamo 27/04/2025 majira ya saa saba mchana huko katika Kijiji na Kata ya Ndirigishi, Tarafa ya Matui Wilaya ya Kiteto na Mkoa wa Manyara. Mwanaume mwenye umri wa miaka 71 Mkulima Mkazi wa Kijiji cha Ndirigishi aliuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na sehemu za siri na mtoto wake, Mwanaume mwenye umri wa miaka 22, Mkulima na mkazi wa Ndirigishi. Mtuhumiwa alikuwa ana ugomvi na baba yake akidai kuwa anamroga kwa kumtupia majini na popobawa na kuwa yanamuingilia kinyume na maumbile hivyo kila wakikaa kama familia kulijadili baba yake huyo anakuwa anamcheka. Mtuhumiwa amekamatwa na amekiri kumuua baba yake mzazi na kumkata sehemu za siri kisha kuhamisha mwili na kuupeleka mbugani na sehemu za siri kuzifukia. Chanzo cha tukio hili ni imani za kishirikina. Mtuhumiwa amekamatwa na kufikishwa mahakamani.

**10. Manyara**

**Mwanafunzi abakwa na kuuawa kwa kuvunjwa shingo kisha kutobolewa macho.**

Mnamo 01/05/2025 majira ya saa tatu asubuhi huko katika Kijiji cha Gidamara Kata ya Gallapo Tarafa na Wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara. Mwanaume mwenye umri wa miaka 46, mkulima na mkazi wa Gidamara aligundua kuuwawa kwa mtoto wake wa kike mwenye umri wa miaka 13, mwanafunzi wa darasa la sita shule ya msingi Yayasea kwa kubakwa, kuvunjwa shingo na kutobolewa macho yake na kitu chenye ncha kali na Mwanaume mwenye umri wa miaka 26, Muiraq mkazi wa Gidamara. Kwa mujibu wa baba yake ni kwamba mwanaye aliondoka nyumbani kwenda shuleni siku ya 29/04/2025 asubuhi na hakurudi tena nyumbani hadi alipokutwa akiwa ameshafariki dunia na mwili wake ukiwa kwenye shamba la mahindi. Chanzo cha tukio hilo ni tamaa ya ngono. Mtuhumiwa amefikishwa mahakamani.

**11. Iringa**

**Baba amuua mtoto wake na kumkatakata vipande, kuponda mifupa yake kisha kumtupa kwenye shimo la choo.**

Mnamo 06/05/2025 majira ya saa nne asubuhi huko Mtaa wa Lukosi - Mtwivila Kata ya Mkwawa, Wilaya na Mkoa wa Iringa. Mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 5, Msagala, Mwanafunzi wa shule ya chekechea Lightness Day Care aliuawa na baba yake mzazi mwenye umri wa miaka 28, Msagala, dereva bodaboda mkazi wa mtaa wa Lukosi - Mtwivila, kwa kuchinjwa na kisu na kisha kukatwakatwa vipande vidogodogo kwa kutenganishwa viungo na kuponda mifupa ya mwili wake kwa kutumia jiwe na kutupwa kwenye shimo la choo lililopo ndani ya nyumba anapoishi. Baada ya kufanya tukio hilo aliendа kuripoti Ofisi ya Dawati la Jinsia Wanawake na Watoto - Polisi Wilaya Iringa taarifa za uongo za kupotea kwa mtoto wake huyo ili kuficha uhalifu alioutenda. Jeshi la Polisi lilipata taarifa za siri kuwa yeye ndiye muuaji na baada ya kuhojiwa alikiri kosa na kwenda kuonyesha mabaki ya mwili wa mtoto yaliyopatikana kwenye shimo la choo. Chanzo ni imani za kishirikina. Mtuhumiwa amekamatwa na kufikishwa mahakamani.

**12. Songwe**

**Auawa kwa kukatwa sehemu mbalimbali na kisha kunyofolewa sehemu za siri.**

Mnamo 23/05/2025 majira ya saa tatu asubuhi huko Kitongoji cha Nkanka Kijiji na Kata ya Itumba, Tarafa ya Bulambya Wilaya ya Ileje Mkoa wa Songwe, Mwanaume mwenye umri wa miaka 54, Mnyiha, mkulima wa Nkanka aliuawa kwa kukatwakatwa na kitu chenye makali kichwani, taya la kulia, kifuani juu ya ziwa la kushoto na kukatwa sehemu za siri(uume) na kutoweka nao na mtu/watu wasiofahamika. Mbinu ni kumvizia akiwa njiani akitokea kilabuni kuelekea nyumbani kwake na kuanza kumshambulia. Chanzo ni imani za kishirikina. Kesi ipo chini ya Upelelezi kubaini watuhumiwa hao.

**13. Mbeya**

**Kuendesha gari kwa uzembe na kusababisha vifo (27) na majeruhi (9).**

Mnamo 07/06/2025 majira ya saa moja na dakika arobaini na saba usiku. Huko eneo la Mlima Iwambi Tarafa ya Utengule Usongwe, Wilaya ya Kipolisi Mbalizi Mkoa wa Mbeya barabara kuu ya Mbeya - Tunduma. Gari yenye namba za usajili T830 EDP/T148 CTD aina ya Lori Scania iliyokuwa ikiendeshwa na Mwanaume mwenye miaka 33, Mmalila, mkazi wa Tunduma ikitokea Dar - es-salaam kuelekea Zambia iligonga magari mawili kwa nyuma ambayo ni T 257 DVP Mistubish Rosa na gari T185 DMF aina ya Toyota Lite Ace na kutumbukia kwenye bonde la mto Mbalizi na kukita kwenye ukingo wa mto na kusababisha vifo vya watu 27 wanawake 12 kati yao watoto 02 na wanaume 15 kati yao watoto 02. Majeruhi ni 09 kati yao wanaume 07, wanawake 02. Chanzo cha ajali ni uzembe wa dereva wa gari namba T.830 EDP/T148 CTD aina ya scania kushindwa kulimudu gari kwenye mteremko. Mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

**14. Kagera**

**Kupatikana na viungo vidhaniwavyo kuwa vya binadamu**

Mnamo 17/06/2025 majira ya saa kumi na moja na nusu, huko Standard Lodge iliyopo Mtaa wa Omkituli, Kata ya Kibeta, Tarafa ya Rwamishenye, Manispaa ya Bukoba, Mkoa wa Kagera. Mwanaume mwenye umri wa miaka 42, Mnyiha, Mganga wa tiba asili, mkazi wa Mbozi Mkoa wa Songwe alikamatwa akiwa na viungo vidhaniwavyo kuwa vya binadamu ambavyo ni kipande kimoja cha mfupa udhaniwao kuwa taya la Binadamu, kipande cha nyama kilichokaushwa kidhaniwacho kuwa moyo wa binadamu, kipande cha nyama kilichokaushwa kidhaniwacho kuwa kondo la uzazi wa binadamu kipande cha nyama kilichokaushwa kidhaniwacho kuwa uke wa mwanamke. Pia alipatikana na vipande viwili vya ngozi viliyokaushwa vidhaniwayo kuwa vya nyoka aina ya chatu, kipande kimoja cha ngozi ya nyoka, pembe mbili za mnyama pori, na vipande vitatu vya mifupa vya mnyama. Sampuli zilichukuliwa na kupelekwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi. Mtuhumiwa alifikishwa mahakamani.

**15. Kilimanjaro**

**Mama mzazi awaua watoto wake wawili kisha na yeye kujichoma kisu.**

Mnamo 20/06/2025 majira ya saa sita na dakika arobaini na tano mchana huko Kitongoji cha Mungushi Kati, Kijiji cha Mungushi, Kata ya Masama Kusini, Zone namba 12, Tarafa ya Masama Wilaya ya Hai Mkoa Kilimanjaro. Watoto wawili wote jinsia ya kike, Wachaga, umri wa miaka 4 na mwingine miezi 06 wakazi wa Mungushi waliuawa kwa kuchomwa na kisu sehemu mbalimbali za miili yao na mama yao mzazi mwenye umri wa miaka 26, Mchaga, mkulima, mkazi wa Mungushi ambaye baada ya tukio hilo naye alijichoma na kisu sehemu za shingoni, kifuani na tumboni. Mtuhumiwa alipelekwa hospitali ya KCMC kwa matibabu. Chanzo cha tukio ni mgogoro wa kifamilia kati ya mtuhumiwa na mume wake. Mtuhumiwa alifikishwa mahakani.

**16. Morogoro**

**Kupatikana kwa viungo vya binadamu**

Mnamo 24/6/2025 majira ya jioni huko katika Kitongoji cha Mkanga Misima, Kijiji, Kata na Tarafa ya Ngoheranga, Wilaya ya Malinyi Mkoa wa Morogoro ilipatikana taarifa ya kuonekana kwa mabaki ya viungo vinavyodhaniwa kuwa ni vya binadamu. ilidhaniwa kuwa ni sehemu ya mwili wa Mwanaume, miaka 30, msukuma, mkulima, mkazi wa Mkanga, ambaye alitoweka tangu April, 2023 ambapo mwili wake ulikutwa kwenye shimo lililochimbwa kwa ajili ya kupasulia mbao jirani na makazi ya watu watatu ambao wote ni watu wenye unasaba naye. Watu hao walikamatwa na kuwa sehemu ya uchunguzi na upelelezi. Baada ya sampuli kuchukuliwa na kupelekwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi majibu yaliwaunganisha watuhumiwa wawili na kosa na kisha walipelekwa mahakamani kwa kosa la mauaji.

## 17. Kilimanjaro

**Kuendesha gari kwa uzembe na kusababisha vifo (42), majeruhi (30) na uharibifu wa vyombo**

Mnamo 28/06/2025 majira ya saa Kumi na moja kamili jioni huko Maeneo ya Sabasaba Kata ya Same Tarafa ya Same Zone Namba 01, Barabara Kuu Moshi Tanga. Gari namba T179 CWL aina ya Fuso Bus mali ya kampuni ya Channel One ikiendeshwa na Mwanaume mwenye Miaka 60, Msambaa mkazi wa Tanga, akitokea Arusha kuelekea Tanga aligongana na Gari namba T199 EFX aina ya Mitsubishi Rosa mali ya kampuni ya Mwami ikiendeshwa na Mwanaume mwenye umri wa miaka 44, Mpare, mkazi wa Same akitokea Same mjini kuelekea Moshi na kusababisha vifo vya watu 42 na majeruhi 30. Chanzo cha ajali ni gari namba T179 CWL Fuso Bus kupasuka tairi la mbele upande wa kulia na gari kuhama kutoka upande wake wa kushoto mwa barabara na kuhamia upande wa kulia mwa barabara kisha kugongana uso kwa uso na gari namba T.199EFX Mistubishi Rosa kupelekea kuwaka moto kwa magari yote mawili huku abiria wakiwemo ndani.

## 18. Dodoma

**Mume amuua mke wake kisha kumtumbukiza kwenye shimo la choo.**

Mnamo 29/06/2025 majira ya saa kumi na mbili kasoro robo jioni, huko Mtaa/Kata ya Mpunguzi, Wilaya na Mkoa wa Dodoma. Mwanamke mwenye umri wa miaka 30, Mgogo, mkulima na mkazi wa Mpunguzi alikutwa akiwa ameuwawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na kisha kutumbukizwa kwenye shimo la choo cha nyumbani kwake na mme wake mwenye umri wa miaka 39, Mgogo, mkulima na mkazi wa Mpunguzi. Baada ya kutekeleza mauaji hayo mtuhumiwa alifika kituo cha Polisi kati Dodoma na kutoa taarifa ya uongo ya kupotelewa na mke wake. Chanzo cha tukio ni wivu wa mapenzi. Mtuhumiwa amefikishwa mahakamani.

# SURA YA SABA

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.0 Utangulizi

Baada ya kuangalia hali halisi ya uhalifu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2025 mapendekezo yametolewa ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi katika kufikia malengo mahususi ya kulinda raia na mali zao, kudumisha amani pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi. Hii itasaidia kujenga mazingira salama kwa wananchi, taasisi na wawekezaji katika uzalishaji mali, shughuli za kijamii na ujenzi wa Taifa kwa ujumla.

## 7.1 Hitimisho

Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, wadau wa ndani na nje pamoja na jamii kwa ujumla katika kupambana na uhalifu nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2025, makosa makubwa ya jinai yamepungua kwa asilimia 11.7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024. Kwa upande wa usalama barabarani, matukio makubwa yamepungua kwa asilimia 27.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024.

Katika kutekeleza majukumu yake, Jeshi la Polisi limepata mafanikio kwa kupunguza uhalifu licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza wajibu wake kwa weledi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mingine. Hivyo, Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali, wadau na jamii kwa ujumla katika kutatua changamoto zinazojitokeza ili kufikia lengo kuu la usalama wa watu na mali zao.